# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

## RIPOTI YA UTAFITI WA SHERIA YA NJIA MBADALA ZA UTATUZI WA MIGOGORO ZANZIBAR, SURA YA 25

## NAMBA 09 /2022

**INAWASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

**JANUARI, 2022**

**MHESHIMIWA HAROUN ALI SULEIMAN,**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA,**

**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI,**
**MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR,**
**ZANZIBAR.**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986, kwa heshima, Tume inawasilisha Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar, Sura ya 25.

**…………………………**

**KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI,**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA,**
**ZANZIBAR**

**27 Juni, 2022.**

## MAKAMISHNA WA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR



**BIBI. KHADIJA SHAMTE MZEE**

**MWENYEKITI**



**DKT.YAHYA KHAMIS HAMAD**
**KAMISHNA**



**ND. SALIM MOHAMED ABDALLA**
**KAMISHNA**



**ND. JUMA MSAFIRI KARIBONA**
**KAMISHNA**



**DKT. SIKUJUA OMAR HAMDAN**
**KAMISHNA**



**MHE. JAJI AZIZA IDDI SUWEDI**
**KAMISHNA**



**ND. MUSSA KOMBO BAKARI**
**KATIBU**

| | |
|---|---|
| Mhe. Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti |
| Mhe. Jaji Aziza Iddi Suwedi | Kamishna |
| Dr. Yahya Khamis Hamad | Kamishna |
| Dr. Sikujuwa Omar Hamdan | Kamishna |
| Nd. Salum Mohammed Abdalla | Kamishna |
| Nd. Juma Msafiri Karibona | Kamishna |
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu |

**WATAFITI**

| | |
|---|---|
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu wa Tume |
| Nd. Yakoub Rajab Juma | Mtafiti wa Sheria |
| Nd. Mariam Rashid Ali | Mtafiti wa Sheria |

Tume ya Kurekebisha Sheria

Vuga, Zanzibar-

P.O BOX 2539,

Simu +255 24 2231143,

Nukushi +255 24 2231137,

barua pepe info@lrcz.go.tz,

tovuti www.lrcz.go.tz

## VIFUNGU VYA UTANGULIZI


**Makamishna……………………………………………………………………………………ii**

**Sheria zilizotumika………………………………………………………………………ix**

**Shukrani………………………………………………………………………………………ix**

**Rejea……………………………………………………………………………………………xii**

**SURA YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**……………………………………………………………………………………..1

1.1 **Mamlaka ya Tume** ya Kurekebisha Sheria Zanzibar……………………………………….1

1.2 Tamko la Utafiti……………………………………………………………………………………2

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiki……………………………………………………………………….3

1.4 Chimbuko la Utafiti………………………………………………………………………………...3

1.6 Historia ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro………………………………………...4

1.7 Njia zilizotumika katika Utafiti…………………………………………………………………6

1.8 Hadidu Rejea……………………………………………………………………………………...7

**SURA YA PILI**

2.0 **MFUMO W SERA NA SHERIA………………………………………………………………8**

**2.1 Mfumo wa Sera………………………………………………………………………………8**

2.1.1 Sera ya Uwekezaji Zanzibar ya mwaka 2005…………………………………………...8

2.1.3 Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020…………………………………………………...8

2.2 Mfumo wa Sheria……………………………………………………………………………...9

2.2.1 Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25…………………………………………………………...9

2.2.2 Sheria ya Usuluhishi(Tunzo za Kigeni)Sura ya 27………………………………………11

2.2.3 Sheria ya Mahusiano Kazini Nam. 1 ya 2005…………………………………………...12

2.2.4 Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8………………………………………………14

2.2.5 Sheria ya Mahkama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahkama Kuu) Nam. 9 ya 2013…………………………………………………………………………………….16

2.2.6 Sheria ya Mahkama ya kadhi Nam. 9 ya 2017…………………………………………18

2.2.7 Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar Nam. 4 ya 2021………………………………19

2.2.8 Sheria ya Mahkama ya Ardhi ya Nam. 7 ya 1994……………………………………………....20

**SURA YA TATU**

3.0 **UTANGULIZI………………………………………………………………………………………21**

3.1 Kutungwa kwa Sheria mpya ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro…………………21

3.2 Kuanzishwa kwa kituo cha Njia Mbadala za utatuzi wa Migogoro Zanzibar (**Zanzibar ADR Centre**)…………………………………………………………………22

3.3 Kuwepo na msimamizi wa utatuzi wa migogoro (regulator)……………………………...22

3.4 Kuanzishwa kwa vyanzo vya fedha za kuendesha shughuli za Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro………………………………………………………………...23

3.5 Kituo kusaji Wasuluhishi na wapatanishi (arbitrators and mediators)…………………23

3.6 Kufungua Ofisi za Kituo katika Ngazi za Mikoa……………………………………………….23

3.7 Wahusika kuwa huru kuchagua idadi ya wasuluhishi wa migogoro…………………....24

3.8 Wahusika kuwa huru kuchagua mahali utakapofanyika ushuluhishi…………………...24

3.9 Mahkama kutoa msaada katika kuchukua ushahidi……………………………………….....24

3.10 Kuwepo kwa utaratibu au muongozo maalum wa kufuatwa katika Kutatua migogoro……………………………………………………………………………………..25

3.11 Kutolewa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutumia njia mbadala Za utatuzi wa migogoro…………………………………………………………………………..26

3.12 Kutunga sheria ya Usuluhishi wa Migogoro ya kibiashara (Commercial Arbitration)………………………………………………………………………....26

3.13 Sheria itakayotungwa izingatie taratibu za njia mbadala za utatuzi wa Migogoro ambazo hazitofanana na taratibu za kimahkama……………………………….26

3.14 Kuweka kifungu maalum ktika sharia kitakachowashurutisha wananchi Kutatua migogoro yao kwa kuanzia na njia mbadala za utatuzi wa migogoro……….27

3.15 Sheria itakayotungwa kutambua ushahidi wa kielektroniki……………………………...27

**SURA YA NNE**

4.0 **MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU WA NCHI MBALI MBALI…………………....28**

4.1 Mikataba ya Kimataifa…………………………………………………………………………...28

4.1.1 Sheria ya Masharti ya usuluhishi (Itifaki) Sura ya 26…………………………………….28

4.1.2 Mkataba wa Umoja wa mataifa (UN Charter) wa 1945………………………………….29

4.1.3 Chama cha Usuluhishi cha Afrika……………………………………………………………..30
4.1.3.1Majukumu ya Chama cha Usuluhishi cha Afrika……………………………………………..31
4.1.3.2 Muundo wa Chama cha Usuluhishi cha Afrika……………………………………………..31
4.1.4 Mwongozo wa Kisheria wa Tume ya Kimataifa ya Biashara chini ya
Umoja wa Mataifa (UNCITRAL) wa 1985……………………………………………………32
4.1.4.1 Idadi ya Wasuluhishi……………………………………………………………………………...33
4.1.4.2 Uwezekano wa Msuluhishi kutokuwa Huru au kuwa na Upendeleo…………………34
4.1.4.3 Uwezo wa kutoa Uamuzi wa Mpito…………………………………………………………....34
4.1.4.4 Kuanza kwa Usuluhishi……………………………………………………………………………..35
4.1.5 Mkataba uliorekebishwa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za
Afrika Magharibi wa 1993……………………………………………………………………....35
4.1.6 Mkataba wa jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wa 1999……………………………....36
4.1.7 Sera ya Uwekezaji wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi ya 2018…………37
4.1.8 Shirika la Kimataifa la hakimiliki (WIPO)………………………………………………….....38
4.1.9 Kituo cha Kikanda cha Cairo cha usuluhishi wa Kimataifa wa Biashara(CRCIA)..45
**4.2 SHERIA NA UZOEFU WA NCHI MBALI MBALI……………………………………………....47**
4.2.1 Jamhuri ya Kenya………………………………………………………………………………….....47
4.2.1.1 Sheria ya Kituo cha Nairobi cha usuluhishi wa Kimataifa Nam. 26 ya 2013……..47
4.2.2 Uzoefu wa Tanzania Bara…………………………………………………………………………48
4.2.2.1 Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Bara Nam.2 ya 2020……………………………....49
4.2.3 Uzoefu wa Nchi ya Ghana……………………………………………………………………….…52
4.2.3.1Sheria ya Njia Mbadala za utatuzi wa Migogoro ya usuluhishi kutoa
Amri chini ya 2010……………………………………………………………………………………..52
4.2.4 Uzoefu wa Nchi ya Mauritius……………………………………………………………......55
4.2.4.1 Sheria ya Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 37 ya 2008……………………………….....55
4.2.5 Uzoefu waq Nchi ya Samoa………………………………………………………………………..57
4.2.6 Uzoefu wa Nchi ya Ufaransa……………………………………………………………………...58
4.2.6.1 Mahkma ya Kimataifa ya usuluhishi ya nchini Ufaransa…………………………………58
4.2.7 Uzoefu wa nchi ya Uingereza………………………………………………………………………60
4.2.7.1 Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro cha London……………………………...60
4.2.7.1.1 Kituo kufanya usuluhishi kwa njia za kimtando……………………………………….....60

**SURA YA TANO**

5.0 **MAPENDEKEZO NA HITIMISHO.................................................................62**

5.1 **MAPENDEKEZO......................................................................................62**

5.1.1 Mapendekezo ya Kisheria..........................................................................62

5.1.1.1 Kutungwa kwa sheria mpya itakayojulikana kama Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar (Zanzibar Aternative Dispute Resolution Act)......62

5.1.1.2 Kuwekwa kwa kifungu makhsusi cha kuanzisha Kituo cha njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar..........................................................66

5.1.1.3 Kuanzishwa kwa Mfuko wa njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro..........................70

5.1.14 Watatuzi wa Migogoro kutokuingiliwa Utendaji wao na maamuzi wanayotoa....70

5.1.1.5 Watatuzi wa Migogoro kupewa uwezo wa kuitisha kielelezo au waraka Wowote unaohusiana na mgogoro..........................................................71

5.1.1.6 Kuweka wajibu kwa wahusika wa mgogoro katika kufuata mionzozo Ya utatuzi wa migogoro..........................................................................71

5.1.1.7 Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro kutokuingilia mifumo Ya Kimahkama..........................................................................................72

5.1.1.8 Kuweka kifungu maalum katika Sheria kitakachowashurutisha wananchi Kutatua mizozo yao kwa kuanzia na njia mbadala za utatuzi wa migogoro........72

5.1.1.9 Upatanishi(Mediation) kutokutawaliwa na utaratibu ulio rasmi(too formal).....73

5.1.1.10 Sheria itakayotungwa kutambua ushahidi wa kielekrtroniki...............................73

5.1.1.11 Sheria iweke utaratibu au muongozo maalum wa kufuatwa katika Kutatua migogoro..........................................................................................74

5.1.1.12 Sheria ibainishe utartibu wa kuwasilisha ombi na kuanza kwa Usuluhishi wa ndani na wa Kimataifa...................................................................74

5.1.1.13 Kurekebishwa kwa Sheria ya mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994......................75

5.1.1.14 Sheria itambue suala la uwekilishaji wa wahusika wa mgogoro..........................76

5.1.1.15 Kuwakilishwa kwa muhusika katika Usuluhishi endepo atafariki, Kufilisika au kumalizika kwake (winding up)..................................................76

5.1.1.16 Watatuzi wa Migogoro kuzingatia maadili....................................................77

5.1.1.17 Msuluhishi kupewa uwezo wa kutoa uamuzi wa mpitio......................................77

5.1.1.18 Sheria iainishe makosa na adhabu..............................................................77

5.1.1.19 Kituo kiweke viwango vya tozo na ada za utatuzi wa migogoro........................78
**5.1.2 Mapendekezo yasiyo ya Kisheria/Kiutendaji...............................................78**
5.1.2.1 Kutungwa kwa sera maalum itakayojulikana kama Sera ya njia Mbadala
Za Utatuzi wa migogoro Zanzibar…………………………………………………………...78
5.1.2.2 Suala la utungaji wa Kanuni………………………………………………………………..79
5.1.2.3 Wajibu wa kutoa eleimu juu ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro
Kwa wananchi…………………………………………………………………………………....79
5.1.2.4 Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar kiwe ni
Jengo lenye hadhi…………………………………………………………………………………80
**5.2 Hitimisho………………………………………………………………………………………..80**

## ORODHA YA SHERIA ZILIZOTUMIKA

### SHERIA ZA ZANZIBAR

- Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25
- Sheria ya Usuluhishi (Tuzo za Kigeni) Sura ya 27
- Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8
- Sheria ya Mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994
- Sheria ya Mahusiano Kazini Nam. 1 ya 2005
- Sheria ya Mahkama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahkama Kuu) Nam. 9 ya 2013
- Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017
- Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar Nam. 4 ya 2021

### SERA NA MIPANGO

Sera ya Uwekezaji Zanzibar ya 2005

Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020

### MIKATABA YA KIMATAIFA

- Sheria ya Masharti ya Usuluhishi (Itifaki) Sura ya 26
- Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter) wa 1945
- Mkataba uliorekebishwa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) wa 1993
- Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wa 1999
- Sera ya Uwekezaji ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi ya 2018

**SHERIA NA UZOEFU WA NCHI MBALI MBALI**

- Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Nam. 30 ya 2007 ya Samoa
- Sheria ya Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 37 ya 2008 ya Mauritius
- Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ya 2010 ya Ghana
- Sheria ya Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 26 ya 2013 ya Kenya
- Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Bara Nam. 2 ya 2020
- Mahkama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya Ufaransa
- Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro cha London

**SHUKRANI**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imefanikiwa kufanya mapitio ya Sheria hii ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro, Sura ya 25 ya Sheria za Zanzibar, kwa ushirikiano mkubwa wa watu na taasisi mbali mbali. Tume inawashkuru sana wote waliosaidia utafiti huu hadi kufikia hatua ya kutayarisha Ripoti hii. Shukrani zetu za dhati ziwaendee Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdallah na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mheshimiwa Mwinyi Talib Haji, kwa msaada na miongozo yao katika mapitio ya Sheria hii. Aidha, kwa dhati tunawashkuru majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar walioshiriki katika kutoa michango yao wakati wa utafiti wa Sheria hii.

Tume pia inawashukuru sana wadau wote walioshiriki katika vikao mbali mbali vya kukusanya maoni yao kuhusiana na Sheria hii. Maoni hayo yanathaminiwa sana kwani yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika utafiti na hatimaye utayarishaji wa Ripoti hii. Wadau hao ni pamoja na Mahakama Kuu ya Zanzibar, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Jumuiya ya Mawakili Zanzibar, ……….

Shukran za pekee ziwaendee Makamishna wa Tume, Katibu wa Tume Nd. Mussa Kombo Bakari na wafanyakazi wa Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuongoza zoezi la utafiti huu na kufanya uchambuzi yakinifu na uandishi na uchapaji wa ripoti hii.

**Ahsanteni sana.**

## REJEA

## TOVUTI


- https://www.lawreform.ie/_fileupload/consultation%20papers/cpadr.pdf
- https://www.arbitrage.org/caip/?lang=en
- https://www.idrc.co.uk/
- https://www.idrc.co.uk/virtual-hybrid-hearings/
- https://www.legalserviceindia.com/legal/article-2308-introduction-to-the-concept-of-alternative-dispute-resolution.html
- https://www.un.org/en/about-us/un-charter
- https://www.wipo.int/amc/en/arbitration/what-is-arb.html
- https://ecowas.int/ecowas-law/treaties/
- https://www.eac.int/overview-of-eac#:~:text=The%20East%20African%20Community%20(EAC,its%20headquarters%20in%20Arusha%2C%20Tanzania.
- https://www.mea.gov.in/Portal/ForeignRelation/east-african-community-april-2011.pdf
- https://en.wikipedia.org/wiki/World_Intellectual_Property_Organization

# RIPOTI YA NJIA MBADALA ZA UTATUZI WA MIGOGORO

## SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Mamlaka ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imeanzishwa chini ya Sheria Namba. 16 ya 1986. Kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria hiyo, Tume ina jukumu la kufanya tafiti, mapitio ya sheria mbali mbali na kupendekeza marekebisho ya sheria hizo. Pamoja na hayo, Tume ina jukumu la kuziboresha sheria kulingana na misingi ya sheria na kwa kuzingatia mipango ya maendeleo ya nchi. Katika kukamilisha jukumu hili, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar hukutana na wadau mbalimbali kwa lengo la kupata maoni na kufahamu kwa kina maeneo yenye changamoto katika utekelezaji wa sheria.

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar katika Mpango kazi wake wa mwaka 2022, miongoni mwa kazi za mapitio iliyojipangia ni kufanya mapitio katika Sheria ya Usuluhishi (Abitration Decree cap 25) na sheria mbali mbali zinazohusiana na taratibu za njia mbadala za utatuzi wa migogoro. Mbali ya kuwepo kwa mpango huo, Tume imefanya mapitio katika eneo hili kufuatia hotuba za Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi Mh. Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye

amekuwa akisisitiza juu ya haja ya kuweka mazingira ya utatuzi wa migogoro kwa haraka, ikiwemo kupitia njia mbadala za utatuzi wa migogoro hiyo.

Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya utafiti kwa mujibu wa kifungu cha 4, 10 na 11 ili kuweza kushauri miongozo, usimamizi, na utaratibu unaotakiwa kutumika katika suala zima la utatuzi wa migogoro na kuweka namna bora za kuanzisha Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ili kurahisisha na kusikiliza kesi kabla kwenda Mahakamani. Katika kufanikisha kazi hiyo, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ilikutana na taasisi zinazohusika na masuala ya upatanishi na usuluhishi wa migogoro ili kupata uwelewa wa taratibu za usuluhishi wa migogoro zinavyofanyika.

**1.2 Lengo la Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuangalia suala la njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika mtizamo wa kisheria na maeneo mengine yasiyo ya kisheria na kutoa mapendekezo Serikalini. Lengo hili linazingatia:

a. Sheria mbali mbali zinazozungumzia masuala ya kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro, ubora na udhaifu na kupendekeza kutungwa kwa sheria mpya ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro Zanzibar;

b. kupendekeza mfumo ulio bora na imara wa kuanzisha Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro; na
c. kupendekeza muundo mzuri zaidi wa vyombo vitakavyosimamia utatuzi wa migogoro nchini.

## 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Pamoja na kuwepo kwa Sheria ya Usuluhishi wa migogoro Zanzibar, kwa namna moja au nyengine, Sheria hiyo inaonekana kuwa haikidhi haja kwa wakati wa hivi sasa. Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inaona kuwa Sheria hiyo haikidhi mahitaji yaliopo na kwamba Sheria hiyo imetungwa toka enzi za utawala wa kikoloni. Hivyo, mazingira yaliyozungumzwa katika Sheria hiyo yanaakisi maisha na utawala wa zama hizo jambo ambalo tumeona ni vyema kufanya mapitio ya Sheria hiyo ili kupendekezwa kutungwa kwa sheria mpya ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro kwa ujumla, ambapo Sheria hiyo itaendana na mazingira ya hivi sasa.

## 1.4 Chimbuko la Utafiti

Chimbuko la utafiti huu ni kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kuona kuwa Sheria ya Usuluhishi wa Migogoro iliyopo haiendani na muda na mazingira ya hivi sasa. Hivyo ikaona ipo haja ya kufanya utafiti huu wa kina ili kuja na suluhishio ambalo litapelekea kutungwa kwa sheria mpya itakayoweka utaratibu

bora wa utatuzi wa migogoro pammoja na njia nyengine mbadala za utatuzi huo. Kama ilivyoelezwa hapo juu, utafiti huu wa sheria pia umefanywa katika eneo hili kufuatia hotuba za Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi ambaye amekuwa akisisitiza juu ya haja ya kuweka mazingira ya utatuzi wa migogoro kwa haraka, kupitia njia mbadala.

## 1.6 Historia ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro

Wazo la Utatuzi wa migogoro kwa kutumia njia mbadala sio jambo geni. Katika karne zilizopita jamii zimekuwa zikitengeneza mifumo isiyo rasmi na isiyo ya kiadui kwa kutatua migogoro. Uwepo wa ushahidi wa matumizi ya mifumo ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro ilibainika katika ustaarabu wa kale wa Misri, Mesopotamia, na Ashuru. Mfumo wa mahakama wenyewe hapo awali ulikuwa ni mfumo mbadala wa utatuzi wa migogoro, kwa maana kwamba ulichukua nafasi ya zamani ya aina za utatuzi wa migogoro, ikijumuisha migogoro inayoibuka kutokana na vita na migogoro mengine.[1]

Katika njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika nyakati zilizopita, moja ya namna ya upatanishi wa mapema zaidi uliowahi kurekodiwa ulitokea zaidi ya miaka elfu nne iliyopita katika jamii ya kale ya Mesopotamia wakati mtawala wa Sumeri alisaidia kuepusha vita na kuendeleza makubaliano katika mgogoro wa ardhi. Vile vile historia inaonesha kuwa mchakato wa utatuzi wa mgogoro kati ya

[1] https://www.lawreform.ie/_fileupload/consultation%20papers/cpadr.pdf

wanaogombana ulikuwa mwingi na muhimu katika jamii ya Mesopotamia. Mnamo karne ya kwanza katika mgogoro uliomhusisha mfanyabiashara, shirika moja lilitetea kwamba migogoro ya kibiashara kutatuliwa nje ya mahakama kupitia mzozo kati ya mdai na mdaiwa kwenye uwepo wa mwamuzi wa tatu. Jukumu la mwamuzi lilikuwa ni kusaidia kurahisisha upatanishi.[2]

Katika njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika ulimwengu wa kimagharibi, pale ambapo mahakama za Athene zilipozidi kujaa, majimbo mbali mbali yalianzisha utaratibu rasmi wa kuwa na msuluhishi wa umma. Wajibu wake wa kwanza msuluhishi huyo ulikuwa ni kujaribu kutatua mgogoro kwa amani. Ikiwa hakufanikiwa, huita mashahidi na kuhitaji kuwasilisha ushahidi kwa maandishi. Hii inaweza kuelezewa kama ni utaratibu wa kisasa wa kutatua mgogoro kwa kuanza na upatanishi kisha usuluhisi (med-arb). Wahusika mara nyingi walishiriki katika mipango ya kina ya kuahirisha maamuzi au kupinga uamuzi wa msuluhishi. Rufaa hupelekwa mbele ya Chuo cha Waamuzi ambao nao huwasilisha suala hilo kwenye mahakama za jadi.[3]

Shairi la kitamaduni la Kigiriki la Iliad, lina mifano kadhaa ya upatanishi na usuluhishi. Mfano mmoja kama huo unahusu mazungumzo ya makubaliano kati ya muuaji na familia ya mwathirika. Sheria ya kitamaduni ilihitaji kwamba mshtakiwa atoe ofa kwa familia ya mwathiriwa ambayo iliwekwa hadharani ili watu wote

[2] https://www.lawreform.ie/_fileupload/consultation%20papers/cpadr.pdf

[3] https://www.lawreform.ie/_fileupload/consultation%20papers/cpadr.pdf

waipime. Hata hivyo, tathmini ya mwisho ya ofa hiyo ilikuwa inafanywa na mzee anayeheshimika ambaye uamuzi wake hukubaliwa na watu wote.[4]

## 1.7 Njia zilizotumika katika utafiti

Katika utafiti huu, njia mbali mbali zimetumika na kusaidia upatikanaji wa taarifa ambazo zimeweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu ikiwemo kufanya mikutano na wadau mbali mbali kutoka Unguja kwa ajili ya kutoa maoni yao. Pia utafiti umejumuisha majadiliano na Taasisi za Kiserikali, Taasisi Binafsi na Asasi za Kiraia kwa lengo la kupata michango yao juu ya suala la njia mbadala za utatuzi wa migogoro na kupitia sheria mbali mbali na rejea ambazo zinazungumzia masuala ya utatuzi wa migogoro kwa kutumia njia mbadala.

Aidha, marejeo ya vitabu, makala na nyaraka mbali mbali zinazozungumzia masuala ya utatuzi mbadala wa migogoro yamepitiwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kwa lengo la kupata uelewa wa sekta hiyo na jinsi inavyofanya kazi na kuweka namna bora ya kuendeleza utawala wa sheria na kuleta maelewano na maafikiano juu ya migogoro mbali mbali inayoibuka katika jamii na sekta mbali mbali za kibiashara, ajira, uchumi na uwekezaji.

## 1.8 Hadidu Rejea

Katika kufanya utafiti huu, Hadidu Rejea zifuatazo zimezingatiwa:

a. kupitia mfumo wa kutatua migogoro kwa njia mbadala;

[4] https://www.lawreform.ie/_fileupload/consultation%20papers/cpadr.pdf

b. kuangalia sheria mbali mbali za Zanzibar zinazohusiana na njia mbadala za utatuzi wa migogoro;
c. kukutana na wadau mbali mbali na kukusanya maoni na mapendekezo yao juu ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro;
d. kuangalia uzoefu wa sheria za nchi mbali mbali ulimwenguni zinazohusiana na njia mbadala za utatuzi wa migogoro;
e. kupitia mikataba ya kimataifa inayohusiana na eneo hili la utafiti;
f. kutoa mapendekezo yanayofaa ya kisheria na kisera; na
g. kukamilisha mapitio ya sheria na kupeleka ripoti serikalini.

# SURA YA PILI

## 2.0 MFUMO WA SERA NA SHERIA

### 2.1 Mfumo wa Sera

#### 2.1.1 Sera ya Uwekezaji Zanzibar ya mwaka 2005

Sera ya Uwekezaji Zanzibar ni sera ambayo kwa kiasi kikubwa imejaribu kutaja na kufafanua kwa kina maeneo mbali mbali ya uwekezaji. Maeneo haya kwa njia moja au nyengine husaidia kwa kiasi kikubwa kuinua sekta mbali mbali za kiuchumi nchini kama vile utalii, viwanda na biashara. Ili kujenga uchumi usioyumba, imara

na endelevu kwa taifa la Zanzibar, mifumo bora ya kisheria inahitaji kuundwa na kusimamiwa ipasavyo hasa katika kuwaongoza vyema wawekezaji pale inapotokezea migogoro katika sekta hiyo ya uwekezaji.

Mifumo ya Kisheria Zanzibar, kupitia Sera ya Uwekezaji Zanzibar ya 2005, haikusita kuainisha utaratibu wa kutatua migogoro. Kwa mujibu wa Sera hii, njia sahihi za kutatua migogoro inayoibuka katika sekta za uwekezaji ikiwemo utalii, viwanda na biashara ni kupitia Usuluhishi na njia ya Kimahkama. Sera hii pia imefafanua kuwa Tanzania ni nchi iliyoridhia na kusaini Mkataba wa Kutambua na Kutekeleza Tunzo za Usuluhishi, na pia ni mwanachama wa Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID).[5]

### 2.1.3 ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2020

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2020-2025 pia inatambua umuhimu wa kuwepo taasisi za utatuzi wa migogoro na kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro kama njia bora za kuzingatiwa na wananchi hasa wafanyakazi katika kutatua migogoro baina yao na waajiri wao. Ilani hii imetaja mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020) ikiwa ni pamoja na kuimarisha taasisi za usuluhishi migogoro kazini.[6]

## 2.2 Mfumo wa Sheria

### 2.2.1 Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25

Miongoni mwa jitihada zilizotumika kusimamia mifumo ya kisheria nchini kwa nyakati hizo ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Usuluhishi ambayo ilitumika kusuluhisha migogoro ambayo sehemu moja ya migogoro hiyo ni Serikali ya

[5] Sera ya Uwekezaji Zanzibar ya 2005, uk 12.
[6] ibara ya 217 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020.

Zanzibar.[7] Miongoni mwa masuala ya msingi yaliyoelezwa katika Sheria hii ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini:

**a) Uwezo wa Msuluhishi kusimamia viapo**

Katika kufanya usuluhishi, Sheria hii imempa uwezo msuluhishi kusimamia viapo kwa wahusika wa mgogoro na mashahidi ambao hutakiwa kutoa ushahidi wao mbele ya msuluhishi, kutaja tunzo au sehemu ya tunzo hiyo katika mfumo wa kesi maalum kwa maoni ya mahkama na kusahihisha kosa katika tunzo, kosa ambalo utendaji wake unatokana na kufanywa kwa bahati mbaya.[8]

**b) Mahkama kuongeza muda wa kutoa tunzo**

Kwa kutambua mamlaka na umuhinu wa Mahkama, Sheria hii imeipa uwezo Mahkama kuongeza muda wa kutoa tunzo (kufanya maamuzi) ya Usuluhishi pale ambapo Mahkama itaona inafaa kufanya hivyo. Katika kufafanua suala hili, Sheria hii inaeleza kuwa muda wa kutoa tunzo, mara kwa mara, unaweza kuongezwa kwa Amri ya Mahkama, ikiwa tunzo hiyo imepitwa au haijapitwa na muda.[9]

**c) Uwezo wa Mahkama kutengua maamuzi ya Msuluhishi**

Kwa kuzingatia kanuni mbali mbali za maadili yanayopasa kuzingatiwa na wasuluhishi wa migogoro wakati wa kutekeleza majukumu yao ya usuluhishi, Sheria hii pia imeipa Mahkama uwezo wa kutengua maamuzi ya msuluhishi ambaye wakati wa kufanya usuluhishi hakuzingatia maadili. Katika kulibainisha suala hili, Sheria hii imeeleza kuwa pale ambapo msuluhishi au mwamuzi hakufuata maadili, au

[7] kifungu cha 1(2), Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25.
[8] kifungu cha 9.Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25.
[9] kifungu cha 12, Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25.

usuluhishi au maamuzi yametolewa vibaya, Mahkama inaweza kutengua maamuzi hayo.[10]

**d) Maamuzi ya Usuluhishi kutekelezwa kama ni Amri ya Mahkama**

Katika kutekeleza maamuzi yaliyotolewa na msuluhishi, Sheria hii imeeleza kuwa ikiwa utekelezaji wa maamuzi hayo utafunguliwa Mahkmani, basi maamuzi hayo yatatekelezwa kama ni Amri ya Mahkama. Kifungu cha 15 cha Sheria hii kinaeleza kuwa tunzo inapowasilishwa Mahkamani kwa mujibu wa masharti yaliyotangulia, (isipokuwa Mahkama itaituma kwa kuzingatiwa na wasuluhishi au mwamuzi, au kuitengua) itatekelezwa kama ni Amri ya Mahkama.

**e) Sharti la Serikali kuwa sehemu ya Mgogoro**

Moja ya maeneo muhimu ya kuzingatiwa wakati wa kufanya mapitio ya Sheria hii ni suala la pande zinazohusika katika mgogoro. Kifungu cha 1(2) cha Sheria hii kinaelekeza kuwa Usuluhishi kwa mujibu wa Sheria hii utafanyika pale tu ambapo mgogoro unahusisha Serikali kama upande unaohusika katika mgogoro huo. Hii ina maana kuwa, endapo Serikali haihusiki katika mgogoro fulani, basi Sheria hii haitotumika katika usuluhishi wa mgogoro huo.

### 2.2.2 Sheria ya Usuluhishi (Tunzo za Kigeni) Sura ya 27

Sheria hii imetumika katika kusimamia tunzo mbali mbali za kigeni na imeanza kutumika rasmi kwa tunzo ambayo imetolewa baada ya mwaka 1924.[11] Matumizi ya Sheria hii pia yanajumuisha ufuatiliaji wa makubaliano ya usuluhishi ambayo itifaki iliyowekwa katika Jadweli la Sheria ya Masharti ya Usuluhishi (Itifaki)

[10] kifungu cha 14, Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25.
[11] kifungu cha 3, Sheria ya Usuluhishi (Tuzo za Kigeni) Sura ya 27.

inatumika na maeneo mengine yaliyotajwa chini ya Sheria hii. Sheria hii imezingatia maeneo ya msingi yafuatayo:

**a) Tunzo ya kigeni kuchukuliwa kuwafunga wahusika wa mgogoro**

Sheria hii imeeleza kuwa tunzo yoyote ya kigeni (foreign award) ambayo itatekelezwa chini ya Sheria hii, itachukuliwa kuwa ni yenye kuwafunga/kuwabana wahusika wote ambao tunzo hiyo imetolewa, na kwa utaratibu maalum, tunzo hiyo inaweza kuegemewa na muhusika yeyote yule kwa namna ya kujilinda au vyenginevyo katika kesi yoyote ya kisheria, na kwa kupitia Sheria hii, tunzo hiyo itatekelezwa.[12]

**b) Masharti ya utekelezaji wa tunzo za kigeni**

Sheria hii imeweka masharti maalum ya kutekelezwa kwa tunzo za kigeni chini ya Sheria hii. Masharti hayo yameeleza kuwa tunzo ni lazima:[13]

i. iwe imefanywa kutokana na kutafuta makubaliano ya usuluhishi ambayo ilikuwa halali chini ya sheria ambayo tunzo hiyo imefanywa;
ii. iwe imefanywa na mahkama (baraza la usuluhishi) na kutolewa kwa mujibu wa makubaliano au kuundwa kwa namna waliyokubaliana wahusika;
iii. iwe imefanywa kwa mujibu wa sheria inayosimamia taratibu za usuluhishi;
iv. iwe ndiyo hatua ya mwisho katika nchi ambayo tunzo hiyo imefanywa; na
v. iwe katika heshima ya jambo ambalo linaweza kupelekwa kwa usuluhishi chini ya sheria ya Himaya.

**2.2.3 Sheria ya Mahusiano Kazini Nam. 1 ya 2005**

[12] kifungu cha 4(2), Sheria ya Usuluhishi (Tuzo za Kigeni) Sura ya 27.
[13] kifungu cha 5, Sheria ya Usuluhishi (Tuzo za Kigeni) Sura ya 27.

Miongoni mwa jitihada zilizofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kulinda na kuweka mfumo bora wa kutatua migogoro katika sehemu za kazi, ni pamoja na kutunga Sheria ya Uhusiano Kazini kupitia Baraza la Wawakilishi. Baraza la Wawakilishi limetunga Sheria hii kwa lengo la kuweka udhibiti mzuri wa mahusiano kazini na kutatua migogoro kati ya waajiriwa na waajiri wao. Sheria hii imeweka taratibu na miundombinu mbali mbali kwa utatuzi bora wa migogoro kama ifuatavyo:

**a) Kuanzisha Kitengo cha Usuluhishi wa migogoro**

Sheria hii imeanzisha Kitengo cha Usuluhishi wa Migogoro kilichopo chini ya Kamisheni ya Kazi ambacho kinaongozwa na Kamishna.[14] Lengo la msingi la Kitengo hiki ni kusimamia migogoro ambayo huibuka baina ya waajiriwa na waajiri wao kwa kusuluhisha au kupatanisha. Hii inajumuisha waajiriwa wote wanaofanya kazi Zanzibar na waajiri wao isipokuwa Majaji na maafisa wengine wa Mahkama, Wajumbe wa Idara Maalum na waajiriwa wa Baraza la Wawakilishi.[15]

**b) Mgogoro wa kazi kufunguliwa katika Kitengo cha Usuluhishi kwa utaratibu maalum**

Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, mgogoro wowote unaohusiana na kazi ni lazima ufunguliwe katika Kitengo cha Usuluhishi wa Migogoro kwa kujazwa fomu maalum.[16] Kamisheni ya Kazi kupitia Kitengo chake cha usuluhishi wa migogoro ndio chombo pekee ambacho, kwa hatua za awali, kina mamlaka ya kisheria kusimamia migogoro inayohusiana na wafanyakazi na waajiri wao.

[14] kifungu cha 72, Sheria ya Mahusiano Kazini Nam. 1 ya 2005.
[15] kifungu cha 2(1)(2), Sheria ya Mahusiano Kazini Nam. 1 ya 2005.
[16] kifungu cha 73(1), Sheria ya Mahusiano ya Kazi, Nam. 1 ya 2005.

Aidha, Sheria ya Mahusiano Kazini imeeleza kuwa mgogoro ambao kwa hatua za awali unafunguliwa katika Kitengo cha Usuluhishi wa Migogoro, hupelekwa kwa Mpatanishi (Mediator) kutoka katika jopo la wapatanishi waliokubaliana.[17] Mgogoro huo hutatuliwa ndani ya siku 30, lakini muda huo unaweza kuongezwa chini ya makubalino ya wahusika. Katika hali ambayo mgogoro umeshindikana kutatulika kwa njia ya Upatanishi, wahusika watakuwa na uwezo wa kuupeleka mgogoro wao katika hatua ya Usuluhishi (Arbitration).[18]

**c) Kuanzishwa kwa Mahkama ya Kazi**

Sheria hii pia imeanzisha Mahkama ya Kazi ambayo ni sehemu ya Mahkama Kuu inayojulikana kama Mahkama ya Kazi Zanzibar.[19] Mahkama hii miongoni mwa mamlaka iliyonayo kisheria ni pamoja na kusikiliza migogoro yote inayohusiana na masuala ya kazi ambayo hupelekwa katika Mahkama hiyo kwa mujibu wa Sheria hii. Mgogoro wowote unaohusiana na mfanyakazi na mwajiri wake unatakiwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa kupelekwa katika Kitengo cha Utatuzi wa Migogoro (DHU) kabla mgogoro huo kupelekwa Mahkama ya Kazi kwa kusikilizwa.

### 2.2.4 Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8

Mbali na kueleza kwa kina taratibu za uendeshaji wa mashauri mbali mbali ya madai, Sheria ya Mwenendo wa Madai imetambua umuhimu wa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro kwa mdai na mdaiwa katika shauri lao. Miongoni mwa maeneo ya misingi yaliyoelezwa katika Sheria hii ni pamoja na:

---

[17] kifungu cha 74(1), Sheria ya Mahusiano ya Kazi Nam. 1 ya 2005.
[18] kifungu cha 75(1), Sheria a Mahusiano ya Kazi Nam. 1 ya 2005.
[19] kifungu cha 80(1), Sheria ya Mahusiano ya Kazi Nam. 1 ya 2005.

**a) Mdai na mdaiwa kukubaliana dai lao kutatuliwa kwa njia ya Usuluhishi**

Sheria hii imezingatia matakwa ya mdai na mdaiwa ya kuridhia shauri lao kutatuliwa kwa njia ya usuluhishi. Katika kuliweka wazi suala hili, Sheria ya Mwenendo wa Madai inaeleza kuwa pale ambapo katika shauri lolote wahusika wamekubaliana kuwa jambo lolote linaloleta tofauti baina yao litapelekwa katika usuluhishi, muda wowote kabla hukumu haijatolewa, wanaweza kuiomba mahkama kwa amri hiyo.[20]

**b) Mdai na mdaiwa kuchagua Msuluhishi**

Baada ya mdai na mdaiwa katika shauri lao liliopo Mahakamani kukubaliana kuwa shauri lao au eneo wanalotofautiana katika shauri hilo lipelekwe kwa Msuluhishi, wahusika hao watapewa fursa ya kuchagua Msuluhishi ambaye wanaona anafaa kusimamia mgogoro wao. Baada ya kuchaguliwa kwa Msuluhishi huyo, Mahkama itaweka muda ambao itaona unafaa kwa Msuluhishi au Mwamuzi huyo kutoa maamuzi au tunzo kwa shauri ambalo analisimamia.[21]

**d) Mahkama kuwa na mamlaka ya kuteua Msuluhishi**

Sheria ya Mwenendo wa Madai imetoa mamlaka kwa mahkama kuteua Msuluhishi au Mwamuzi katika mazingira yafuatayo:[22]

a. ikiwa wahusika wameshindwa kukubaliana ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa uteuzi wa msuluhishi, au mtu, aliyeteuliwa amekataa kuchukua nafasi ya usuluhishi;
b. ikiwa Msuluhishi au Mwamuzi-
    i. amefariki,

[20] kifungu cha 1(1), Jadweli ya tatu, Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8, uk 350.
[21] kifungu cha 2, Jadweli ya tatu, Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8, uk 350.
[22] kifungu cha 5(1), Jadweli ya tatu, Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8, uk 350.

ii. amekataa au amedharau kuwa msuluhishi au amekuwa hana uwezo wa kuwa msuluhisi, au

iii. ameondoka Zanzibar katika mazingira ambayo yataonesha kwamba kurudi kwake kutachelewa;

c. ikiwa wasuluhishi wamepewa uwezo wa kuteuwa mwamuzi lakini wameshindwa kufanya hivyo.

**e) Kuweka kumbukumbu ya maamuzi ya Msuluhishi**

Sheria hii pia imetambua umuhimu wa kuweka kumbukumbu ya maamuzi yanayotokana na jitihada na makubaliano ya pamoja kwa wahusika na kuelekeza kuwa katika tunzo au maamuzi yaliyofikiwa katika shauri husika, watu ambao wametoa maamuzi hayo watatia sahihi zao na kuwasilisha mahakamani malipo na nyaraka ambazo zimechukuliwa na kuthibitishwa mbele yao, na taarifa ya kuwasilishwa mahakamani watapewa wahusika[23].

**2.2.5 Sheria ya Mahkama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahkama Kuu) Nam. 9 ya 2013**

Kutokana na kukua kwa kasi kwa sekta ya biashara nchini na duniani kwa ujumla, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia chombo chake cha kutunga sheria cha Baraza la Wawakilishi kilitunga sheria maalum inayojulikana kama Sheria ya Mahkama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahkama Kuu) Nam. 9 ya 2013. Sheria hii inasimamiwa na divisheni maalum ya Mahkama Kuu Zanzibar (High Court Division) ambapo lengo lake la msingi ni kuitekeleza Sheria hii ikiwemo kusimamia na kutoa maamuzi kufuatia mashauri mbali mbali yanayofunguliwa Mahkamani hapo. Licha ya kusimamia mashauri mbali mbali ya kibiashara kwa

[23] kifungu cha 11, Jadweli ya tatu, Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8, uk 351.

taratibu za kimahkama, Sheria hii imejaribu kusisitiza kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro ikiwemo:

**a) Sheria kutambua umuhimu wa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro**

Sheria ya Mahkama ya Biashara Zanzibar imetambua umuhimu wa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro kwa kueleza kuwa ikiwa shauri halijatatuliwa au kuondoshwa chini ya masharti ya vifungu vya 13, 14, 15 na 16 vyenye kuelezea kuhusu kukutana kabla ya kuanza kwa kesi (pre-trial conference) Mahkama itawaelekeza wahusika wa mgogoro kuwasilisha shauri lao kwa Upatanishi. Baada ya kutoa amri hiyo, Mahkama itachagua Mpatanishi ambaye atatoa tarehe ya kuanza kwa Upatanishi isipokua wahusika kwa pamoja wamewasilisha tamko kwamba Upatanishi haufai.[24]

**b) Kubainisha wajibu wa Mpatanishi (Mediator)**

Sheria hii imempa majukumu mbali mbali Mpatanishi wakati wa kufanya Upatanishi. Miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na:[25]

a. kwa njia ya kujitegemea na bila ya upendeleo, kufanya kila kilichokuwa muhimu kuwasaidia wahusika wa mgogoro kutatua mgogoro wao;
b. pale atakapoona inafaa, anaweza kufafanya mikutano na wahusika kwa pamoja au mmoja mmoja na anaweza kutoa mapendekezo ya utatuzi wa mzozo husika;
c. pale ambapo huduma ya mtaalamu inaweza kupatikana bila ya gharama, au huduma hiyo inaweza kupatikana kwa gharama, na ikiwa wahusika wamekubali kulipa gharama hizo, anaweza kupata ushauri wa mtaalamu

[24] kifungu cha 18, Sheria ya Mahkama ya Biashara Nam. 9 ya 2013.
[25] kifungu cha 23(2), Sheria ya Mahkama ya Biashara Nam. 9 ya 2013.

kuhusiana na vipengele vya utaalamu vya mgogoro ambapo ushauri utatolewa kwa namna ya kujitegemea na bila ya upendeleo;

d. kuongozwa na misingi ya usawa, haki na kutokuwa na upendeleo, na kuzingatia, pamoja na mambo mengine:
    i. haki na wajibu wa wahusika wa mgogoro;
    ii. mwenendo wa biashara husika; na
    iii. mazingira yanayozunguka mgogoro, ikijumuisha mienendo iliyopita baina ya wahusika;
e. katika hatua yoyote ya uendeshaji wa Upatanishi, na katika namna ambayo Mpatanishi ataona inafaa, anaweza kuzingatia matakwa ya wahusika, ikiwemo ombi lolote linalofanywa na muhusika yeyote kati yao la kumtaka Mpatanishi kusikiliza maelezo ya mdomo ili kurahisisha mgogoro kumalizika haraka; na
f. katika hatua yoyote ya uendeshaji wa Upatanishi, kutoa mapendekezo ya utatuzi wa mgogoro.

### 2.2.6 Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017

**a) Mahkama ya Kadhi kuwashauri wahusika kuwasilisha shauri lao kwa upatanishi**

Sheria hii ya Mahkama ya Kadhi imetambua njia mbadala za utatuzi wa migogoro kama ni njia muhimu kwa hatua za awali kutumiwa na pande za mgogoro katika kutatua mgogoro wao. Kabla ya kusikilizwa kwa madai yanayofunguliwa mahakamani hapo kwa taratibu za kimahkama, Sheria hii imempa mamlaka Kadhi kuwashauri na kuwaelekeza wadai na wadaiwa kuwasilisha dai lao kwa pamoja katika taratibu za upatanishi. Sheria hii pia imeeleza kuwa Mahkama ya Kadhi inaweza kuwaelekeza wahusika kuwasilisha shauri lao kwa upatanishi na baada ya

kutolewa kwa amri hiyo, Mahkama itateua Mpatanishi ambaye atapanga tarehe ya kuanza kwa upatanishi isipokuwa wahusika wakitoa tamko rasmi kuwa upatanishi haufai.[26]

Aidha, Sheria imetambua haki ya upatanishi kwa wahusika pale ilipoeleza kuwa wakati wa upatanishi, wahusika wa mgogoro watakuwa na haki ya kutatua jambo lotole kwa kuzingatia suala lililowasilishwa kwa upatanishi.[27] Hivyo, suala la upatanishi kwa mujibu wa kifungu hicho ni haki ya pande zenye mzozo kuamua kama wanahitaji kuingia kwenye upatanishi au vyenginevyo, na hawawezi kushurutishwa katika upatanishi.

**b) Upatanishi unaposhindikana**

Kwa kutambua kuwepo kwa uwezekano wa upatanishi kushindikana, Sheria imeweka utaratibu wa kurudisha mzozo kwa kadhi ili hatua za kusikiliza mzozo huo ziendelee. Hivyo, katika namna ambayo mchakato wa upatanishi umefanyika lakini imeshindikana mgogoro kutatuliwa kwa njia hiyo, Sheria hii imeelekeza kuwa suala litapelekwa kwa Kadhi ambaye ataendelea na shauri kuanzia pale ambapo suala hilo lilipelekwa kwenye upatanishi.[28]

### 2.2.7 Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar Nam. 4 ya 2021

Zanzibar ni visiwa ambavyo wakaazi wake wanafuata itikadi tofauti za kidini. Wapo waislamu (ambao ndio asilimia kubwa ya wakaazi hao) na wasiokuwa waislamu.

[26] kifungu cha 20(1),Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017.
[27] kifungu cha 22(1), Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017.
[28] kifungu cha 17, Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017.

Suala la utatuzi wa migogoro baina ya watu wenye itikadi hizi limeelezwa katika Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar. Sheria imeeleza:

**a) Uwezo wa Mufti kutatua migogoro baina ya watu wa itikadi tofauti za kidini**

Sheria hii imeipa jukumu Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kutatua mgogoro wowote kwa matukio baina ya waislamu wenyewe, waislamu na wasiokuwa waislamu, na makundi ya kiislamu na taasisi mbali mbali.[29] Pia Sheria hii imeeleza kuwa katika kutekeleza jukumu lao la kutatua migogoro baina ya waislamu na wasiokuwa waislamu, Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar inaweza kushirikiana na viongozi wengine wa kidini ambao sio waislamu pamoja na tasisi nyengine.[30]

### 2.2.8 Sheria ya Mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994

Mahkama ya Ardhi ni mahkama ambayo imeanzishwa mwaka 1994 chini ya Sheria ya Mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994. Lengo la msingi la kuanzishwa kwa mahkama hii ni kusikiliza migogoro inayohusiana na ardhi. Mahkama ya ardhi ina mamlaka ya msingi juu ya kesi zilizofunguliwa pale ambapo wahusika wana madai yanayokinzana kuhusiana na ardhi.[31]

Sheria hii imetambua haja ya kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika kusikiliza madai ya wahusika wa mgogoro ambayo yanahusiana na ardhi kama ifuatavyo:

**a) Wahusika katika shauri kupewa fursa ya kuchagua shauri lao kuendeshwa kwa njia ya upatanishi (Mediation)**

[29] kifungu cha 25(1), Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar Nam. 4 ya 2021.
[30] kifungu cha 25(2), Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar Nam. 4 ya 2021.
[31] kifungu cha 13, Sheria ya Mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994.

Wahusika wa mgogoro wamepewa fursa chini ya Sheria hii kuchagua shauri hilo kuendeshwa kwa njia ya upatanishi katika hatua yoyote ya shauri husika. Sheria hii imeeleza kuwa wahusika watatumia upatanishi katika hatua yoyote ya kesi na ikiwezekana, kwa kushirikiana na Mwenyekiti, watafupisha kesi na mashauri ili kupunguza muda wa mchakato wa usikilizaji.[32]

# SURA YA TATU

# MAONI YA WADAU

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea maoni ya wadau kuhusiana na njia mbadala za utatuzi wa migogoro. Maoni ya wadau na mapendekezo yao yalikusanywa katika vikao mbali mbali vilivyoitishwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar. Wadau wengi walichangia kuhusu njia mbadala za utatuzi wa migogoro na kupendekeza maeneo ambayo yatachangia katika kuleta mabadiliko makubwa kwenye Sheria. Wadau walichangia kwa kuonesha umuhimu wa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika migogoro ambayo haina ulazima wa kutatuliwa kwa kufungua shauri mahkamani na kuendeshwa kwa taratibu za kikawaida za uendeshaji wa kesi ambazo zinatumiwa na mahkama husika. Hivyo, Maoni ya wadau yalikuwa kama ifuatavyo;

## 3.1 Kutungwa kwa Sheria mpya ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro

Wadau wamependekeza kutungwa kwa sheria maalum inayojulikana kama Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar. Sheria hii itoe mwelekeo bora

[32] kifungu cha 14, Sheria ya Mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994.

kwa jamii katika kutatua migogoro mbali mbali inayoibuka katika jamii hizo kwa njia zisizokuwa za kimahkama. Sheria iweke utaratibu maalum ambao utawaongoza wananchi kutatua migogoro baina yao ambayo inatokana na masuala ya kibiashara, kazi, uchumi na uwekezaji. Aidha, Sheria hii ibainishe njia mbali mbali za utatuzi wa migogoro ambazo wananchi wa Zanzibar pamoja na wageni wanaweza kuchagua kutumia katika kutatua migogoro yao. Vile vile, Sheria iweke utaratibu mzuri wa utolewaji wa tunzo, kueleza namna bora ambazo tunzo hiyo inasimamiwa pamoja na kuzingatia mambo mengine yote yanayohusiana na njia mbadala za utatuzi wa migogoro.

**3.2 Kuanzishwa kwa kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar (Zanzibar ADR Centre)**

Wadau wamependekeza kuanzishwa kwa Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar ili kutoa huduma bora na za pamoja kwa jamii kuhusiana na migogoro inayoibuka katika jamii hizo. Kituo hicho kitasimamia njia mbali mbali za utatuzi wa migogoro ikiwemo usuluhishi (arbitration), upatanishi (mediation) na mazungumzo (negotiation). Aidha, Kituo hicho kimependekezwa kuwa na wataalamu wa usuluhishi wa migogoro ya aina tofauti ikiwemo migogoro ya biashara, migogoro ya kazi, migogoro ya ndoa na talaka, migogoro ya ardhi, uchumi na uwekezaji.

**3.3 Kuwepo na msimamizi wa utatuzi wa migogoro (regulator)**

Wadau wamependekeza kuwa Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar kitakachoanzishwa chini ya Sheria hii, kiwe na msimamizi (Regulator) wa

masuala hayo ya utatuzi wa migogoro. Msimamizi huyo atakuwa na jukumu la kutoa miongozo na maelekezo juu ya masuala mbali mbali ya utatuzi wa migogoro.

**3.4 Kuanzishwa kwa vyanzo vya fedha za kuendesha shughuli za Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro**

Wadau wamependekeza kuanzishwa kwa vyanzo vya fedha za kuendesha shughuli mbali mbali za kiofisi katika kutatua migogoro. Wadau hao wamependekeza kuwa, ili kuweka misingi imara kwa vyanzo vya fedha, ni muhimu Sheria hiyo mpya ikavitambua vyanzo hivyo. Miongoni mwa vyanzo hivyo vya fedha ni pamoja na ruzuku kutoka Serikalini, tozo na ada zinazokusanywa na Kituo katika kutekeleza majukumu yake, na michango na zawadi kutoka kwa Umma, Taasisi na Jumuiya. Fedha hizo zitumike kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiofisi ikiwemo kutoa elimu kwa umma kuhusiana na njia mbadala za utatuzi wa migogoro, kufanya tafiti na mafunzo mbali mbali yanayohusiana na kazi za Kituo, maendeleo ya rasilimali watu kwa ajili ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro, shughuli nyengine yoyote ambayo Sheria itaelekeza.

**3.5 Kituo kusajili Wasuluhishi na Wapatanishi (arbitrators and mediators)**

Wadau pia wamependekeza kuwa Sheria itakayotungwa ibainishe mtu mwenye sifa aweze kufanya maombi ya kusajiliwa na Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar kama ni Msuluhishi au Mpatanishi. Katika kufanya usajili huo, Kituo kitatunza kumbukumbu katika Daftari la Usajili, majina, anuani na taarifa nyengine za mtu aliyesajiliwa na Kituo kama Msuluhishi au Mpatanishi.

### 3.6 Kufungua Ofisi za Kituo katika Ngazi za Mikoa

Baadhi ya wadau wamependekeza kuwa Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro kifungue vituo visaidizi ambavyo vitafanya kazi za kutatua migogoro katika mikoa tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kufanya hivyo kutasaidia Kituo kuondokana na mashauri ambayo yasingeweza kutatuliwa ndani ya wakati na kusaidia kuoa muda na gharama.

### 3.7 Wahusika kuwa huru kuchagua idadi ya wasuluhishi wa migogoro

Wadau wamependekeza kuwa wahusika katika mgogoro wapewe fursa ya kuchagua wasuluhishi wa mgogoro wao kwa kuzingatia kwamba idadi ya wasuluhishi hao itakuwa nambari isiyo sawa. Aidha imependekezwa kuwa wahusika wakubaliane kuweka utaratibu ambao utatumika katika kuchagua wasuluhishi. Ikiwa wahusika watashindwa kukubaliana kuweka utaratibu huo, utaratibu wa kisheria unaongoza namna ya kuchagua wasuluhishi utatumika.

### 3.8 Wahusika kuwa huru kuchagua mahali utakapofanyika usuluhishi

Kwa upande mwengine, wadau wamependekeza kuwa katika usuluhishi wa migogoro, wahusika wanaozozana wapewe uhuru wa kuchagua mahali wanapopenda ambapo patatumika kusuluhisha mgogoro wao. Ikiwa wahusika wameshindwa kukubaliana juu ya mahali ambapo usuluhishi wa mgogoro wao utafanyika, Baraza la Usuluhishi kwa kuzingatia gharama, mazingira ya shauri husika na wepesi wa wahusika, lichague mahali pa usuluhishi.

### 3.9 Mahkama kutoa msaada katika kuchukua ushahidi

Wadau wamependekeza kuwa Baraza la usuluhishi, au muhusika aliyeidhinishwa na Baraza la usuluhishi, aweze kuiomba msaada Mahkama katika kuchukua ushahidi kwa kufungua ombi maalum mahakamani lenye kujumuisha wahusika wa mgogoro, na hali au aina ya mgogoro uliojitokeza. Aidha, wadau pia wamependekeza kuwa, Mahkama iweze kutekeleza ombi ndani ya mamlaka yake na kwa mujibu wa Kanuni zake za kuchukua ushahidi.

### 3.10 Kuwepo kwa utaratibu au muongozo maalum wa kufuatwa katika kutatua migogoro.

Wadau wamependekeza kuwa masuala ya utatuzi wa migogoro yaekewe utaratibu maalum na wa pamoja ambao kila chombo chenye mamlaka kisheria kutatua migogoro, kilazimike kufuata utaratibu huo, kwa vile vyombo vinavyojishughulisha na kutatua migogoro kwa njia mbadala vilivyopo hivi sasa vinatumia utaratibu uliojiwekea wenyewe. Utaratibu huo utakaowekwa uzingatie mambo yafuatayo:

a) muda wa kusikiliza mgogoro hadi kufikia maamuzi katika upatanishi ambao hautazidi miezi sita, badala ya muda uliozoeleka wa siku thelathini;

b) mawakili kuendelea kuruhusiwa kuingia katika upatanishi (mediation) kama ilivyo hivi sasa;

c) kufungua shauri nje ya muda;

d) na msuluhishi kupewa uwezo kisheria kumuita mtu yeyote ambae anaona anafaa kusaidia ili msuluhishi kufikia maamuzi.

### 3.11 Kutolewa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro

Kutokana na kukosa uelewa wa kutosha kwa jamii za wazanzibari kuhusiana na masuala mbali mbali ya utatuzi wa migogoro kupitia njia mbadala na umuhimu wake, wadau wamependekeza kutolewa elimu kwa umma kuhusu njia mbadala za utatuzi wa migogoro. Maoni hayo ya wadau yanatokana na ukweli kuwa jamii hizo huingia gharama na kupoteza muda mwingi wa kufungua mashauri mahkamani na hatimaye kuchukua muda mrefu mashauri hayo mpaka kumalizika kwake. Hivyo wadau wamependekeza kuwa ili masuala ya utatuzi wa migogoro kwa njia sahihi na yenye kukubalika kisheria yaweze kujulikana na wananchi, ni vyema kuwapatia elimu ya kutosha wananchi hao na kuwajengea uelewa wa kutumia njia hizo.

### 3.12 Kutunga sheria ya usuluhishi wa migogoro ya kibiashara (Commercial Arbitration)

Baadhi ya wadau wameona kuwa kutokana na azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kupunguza mrundikano wa kesi hasa za wawekezaji katika masuala ya biashara, ni vyema sheria itakayotungwa iwe ni kwa ajli ya usuluhishi wa migogoro ya kibiashara tu.

### 3.13 Sheria itakayotungwa izingatie taratibu za njia mbadala za utatuzi wa migogoro ambazo hazitofanana na taratibu za kimahkama.

Wadau wameeleza kuwa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala hufuata misingi na taratibu maalum ambazo huwa ni tofauti na taratibu zinazotumika mahkamani. Hivyo, wadau wamependekeza taratibu za njia mbadala za utatuzi wa migogoro

zisifanane na taratibu za kimahkama. Miongoni mwa taratibu hizo ni pamoja na suala la utambulisho, kueleza maana na faida za upatanishi na kueleza namna itakavyofanyika na muda utakaotumia, maelezo ya ufunguzi na uwasilishaji wa hoja, kuleta nyaraka au vielelezo vya ushahidi, na kutoa maelezo ya ufungaji (tunzo).

### 3.14 Kuweka kifungu maalum katika sheria kitakachowashurutisha wananchi kutatua migogoro yao kwa kuanzia na njia mbadala za utatuzi wa migogoro

Kutokana na kufunguliwa kwa mashauri mengi katika mahkama mbali mbali za Zanzibar na kusababisha mashauri hayo kutokupatiwa ufumbuzi wa kimahkama ndani ya wakati, wadau wamependekeza kuwa Sheria itakayotungwa iweke kifungu kitakachowashurutisha wananchi kutatua migogoro yao kwa njia mbadala za utatuzi wa migogoro kabla ya kufungua madai yao mahkamani. Kuwepo kwa utaratibu huu kutasaidia kupunguza mrundikano wa kesi katika mahakama za Zanzibar na kutapelekea usimamizi bora wa haki ambazo zitapatikana ndani ya wakati.

### 3.15 Sheria itakayotungwa kutambua ushahidi wa kielektroniki

Wadau wamependekeza kuwa Sheria ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro itakayotungwa itambue namna ya kuchukua ushahidi kwa njia za kisasa za kielektroniki. Wadau hao wameeleza kuwa, kutokana na mabadiliko na ukuaji wa kasi wa sayansi na teknolojia, ni muhimu kwa watatuzi wa migogoro kuwekewa mifumo imara na salama ya kisheria ambayo itaendana na kasi ya mabadiliko hayo katika kuchukua ushahidi wa kielektroniki.

# SURA YA NNE

## 4.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU WA NCHI MBALI MBALI

### 4.1 Mikataba ya Kimataifa

Usuluhishi wa kimataifa unatawaliwa na makubaliano ya kibinafsi ya pande zote mbili lakini pia na idadi ya mikataba ya kimataifa ya usuluhishi ambayo inatumika bila ya makubaliano ya wahusika.

### 4.1.1 Sheria ya Masharti ya Usuluhishi (Itifaki) Sura ya 26

Lengo kuu la Sheria hii ni kutekeleza matakwa ya Itifaki za masharti ya Usuluhishi yaliyosainiwa katika mkutano wa Bunge la Umoja wa Mataifa uliofanywa tarehe 24 Septemba 1923. Masharti ya Itifaki hii yanazingatia ngazi za kimataifa pale ambapo nchi zinazoingia katika mikataba hutambua uhalali wa makubaliano yao na pale ambapo hutokea tofauti au migogoro baina yao, huziwasilisha tofauti hizo kwa hatua za Usuluhishi.

Migogoro inayotokana na kwenda kinyume na mikataba inayohusiana na masuala ya kibiashara au jambo jengine lolote linaloweza kutatuliwa kwa njia ya usuluhishi, basi usuluhishi wake utafanyika katika nchi ambayo mamlaka yake hakuna upande wowote unaohusika.[33] Kila nchi ambayo inaingia katika mikataba, inahifadhi haki na wajibu unaotokana na mikataba inayochukuwaliwa kuwa ni ya kibiashara chini ya sheria ya kitaifa.

Aidha, masharti ya Itifaki hizi yamejaribu kueleza taratibu za usuluhishi kwa kufafanua kuwa utaratibu wa usuluhishi, ikiwa ni pamoja na katiba ya baraza la usuluhishi, utaongozwa na matakwa ya wahusika, na kwa sheria ya nchi ambayo usuluhishi unafanyika. Nchi zinazoingia kwenye mkataba zinakubali kuwezesha hatua zote zinazopasa kuchukuliwa katika utaratibu unaohitajika katika maeneo yao

[33] itifaki ya 1 ya Masharti ya Usuluhishi, Jaweli, Sura ya 26.

husika, kwa mujibu wa masharti ya sheria zao zinazosimamia taratibu za usuluhishi ambazo hutumika katika mgogoro husika.[34]

Itifaki hizi pia zimezingatia namna bora za utekelezaji wa maamuzi (tunzo) za usuluhishi, kwa kuzitaka nchi zinazoingia katika makubaliano kujitolea kuhakikisha utekelezaji bora wa mamlaka yao, na kwa majibu wa masharti ya sheria zao za kitaifa, kwa tunzo za usuluhishi  zinazotolewa katika maeneo yao chini ya vifungu vilivyotangulia.[35]

### 4.1.2 Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter) wa 1945

Mkataba wa Umoja wa Mataifa ni Hati iliyoanzishwa na Umoja wa Mataifa ambayo imesainiwa tarehe 26 Juni 1945 huko San Fransisco katika hitimisho la mkutano wa Umoja huo. Hati hii ilianza kutumika tarehe 24 Oktoba 1945. Kwa mujibu wa Hati hii, Umoja wa Mataifa unaweza kuchukua hatua katika masuala mbali mbali kutokana na hadhi yake ya kipekee ya kimataifa na mamlaka yaliyomo katika Mkataba wake, ambao unachukuliwa kuwa mkataba wa kimataifa.[36]

Mkataba wa Umoja wa Mataifa ni chombo cha sheria za kimataifa na nchi wanachama zinafungwa kuzifuata sheria hizo. Tanzania, ikiwemo Zanzibar kama ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa, inalazimika kufuata kikamilifu masharti ya sheria za  kimataifa ambayo yameelezwa katika Hati ya Mkataba wa Umoja huo.

[34] itifaki ya 2 ya Masharti ya Usuluhishi, Jadweli, Sura ya 26.
[35] itifaki ya 3 ya Masharti ya Usuluhishi, Jadweli, Sura ya 26.
[36] https://www.un.org/en/about-us/un-charter

Mkataba wa Umoja wa Mataifa umetambua haja kwa wananchi wa nchi wanachama wa Umoja huo kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro, kwa kueleza kuwa katika hali ambayo inaonekana kuhatarisha utunzaji wa amani na usalama wa kimataifa, wahusika wa mgogoro wowote, kwanza kabisa, watatafuta suluhisho kwa njia ya mazungumzo, uchunguzi, upatanishi, usuluhishi, njia ya kimahkama, kupitia mashirika ya kikanda au mipangilio mengine au njia nyengine yoyote ya amani ambayo wahusika watachagua wenyewe.[37]

### 4.1.3 Chama cha Usuluhishi cha Afrika

Chama cha Usuluhishi cha Afrika (The African Arbitration Association (AAA)) ni taasisi isiyo ya faida iliyoanzishwa katika Bara la Afrika kwa ajili ya kuhuisha shughuli za usuluhishi wa migogoro na njia nyengine za utatuzi wa migogoro katika bara hili.[38] Chama hiki kimekuwa na mchango mkubwa katika upatikanaji wa taarifa kuhusu usuluhishi wa migogoro ya kimataifa inayojitokeza ndani ya Afrika. AfAA kimezikusanya pamoja taasisi 71 za Usuluhishi ndani ya Afrika. Makao makuu ya Chama hiki yapo nchini Rwanda, katika Kituo cha Usuluhishi cha Kigali.

#### 4.1.3.1 Majukumu ya Chama cha Usuluhishi cha Afrika

Chama hiki kina majukumu yafuatayo:

a) Kuratibu shughuli za usuluhishi wa migogoro na njia nyengine za utatuzi wa migogoro kimataifa ndani ya Afrika;
b) Kutoa fursa kwa watatuzi wa migogoro kupata taarifa zinazohusu usuluhishi na njia nyengine za utatuzi wa migogoro;

[37] Ibara ya 33(1) ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa 1945.
[38] African Arbitration Association (AfAA) and International Arbitration in Africa – The Arbitrator

c) Kuwainua wasuluhishi wa kimataifa waliopo Afrika na taasisi za usuluhishi wa migogoro ndani na nje ya Afrika;
d) Kusaidia uratibu wa uteuzi wa wasuluhishi na kuwatumia wasuluhishi na taasisi za usuluhishi za Afrika katika migogoro mbali mbali;
e) Kusaidia kutoa mafunzo ya kitaalam, kujenga uelewa na kujenga uwezo kwa Serikali za Afrika ili kuimarisha mifumo ya sheria katika eneo hilo la utatuzi wa migogoro; na
f) Kuhamasisha ushirikiano baina ya taasisi za utatuzi wa migogoro na taasisi za kielimu katika bara la Afrika.

#### 4.1.3.2 Muundo wa Chama cha Usuluhishi cha Afrika

Chama cha Usuluhishi cha Afrika kinaundwa na Mkutano Mkuu wa Chama ambacho ndiyo chombo cha juu kabisa cha Chama hicho, Bodi ya Wakurugenzi na Sekretarieti ya Chama ambayo huendesha shughuli za kila siku za Chama, chini ya uongozi wa Katibu Mkuu. Bodi ya Wakurugenzi hutoa miongozo ya namna Chama hicho kinavyopaswa kuendeshwa. Ili kujenga uweledi katika Chama hicho, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi hupatikana miongoni mwa wataalamu wa usuluhishi.

### 4.1.4 Mwongozo wa Kisheria wa Tume ya Kimataifa ya Biashara chini ya Umoja wa Mataifa (UNCITRAL) wa 1985

Tume ya Kimataifa ya Biashara chini ya Umoja wa Mataifa (UNCITRAL) imetoa Muongozo wa Usuluhishi wa Kimataifa katika biashara (UNCITRAL Model Law on International Commercial Arbitration 1985 With amendments as adopted in 2006). Mwongozo huo wa Sheria umepitishwa kwa Azimio Namba 40/72 la Umoja

wa Mataifa, mwaka 1985 na mnamo mwaka 2006, Mwongozo huo ulifanyiwa Marekebisho. Mwongozo huo wa kisheria unasisitizwa kuzingatiwa na nchi zote wanachama wakati wa kutunga sheria zao za usuluhishi.[39] Aidha, Chama cha Usuluhishi cha Afrika kimebainisha katika tafiti zake kuwa, miongoni mwa changamoto za Usuluhishi katika bara la Afrika ni sheria za Usuluhishi za baadhi ya nchi kutozingatia Muongozo huo wa UNICITRAL na hivyo, kuwepo kwa tofauti baina ya Sheria za nchi mbali mbali za Afrika katika utungaji wa sharia za Usuluhishi.[40]

UNCITRAL imetoa tafsiri ya Usuluhishi wa Kimataifa wa Kibiashara kwa kueleza kuwa Usuluhishi huo utakuwa wa kimataifa ikiwa pande zinazohusika katika mkataba wa biashara zimekubaliana kuwa mkataba huo unahusisha nchi zaidi ya moja, au wahusika wanatoka mataifa tofauti, au usuluhishi utafanyika nje ya nchi.[41]

Mwongozo huu wa UNCITRAL pia umetafsiri Mkataba wa Usuluhishi ukiwa na maana ya Mkataba baina ya wahusika katika Mkataba kukubaliana kuwasilisha mgogoro au sehemu ya mgogoro baina yao, unaotokana na uhusiano wao kisheria, mbele ya Msuluhishi.[42] Kwa mujibu wa Ibara hiyo ya Mwongozo wa UNCITRAL, Mkataba wa Usuluhishi unapaswa kuwa wa maandishi, ikijumuisha pia kurekodiwa kwa njia ya kielektroniki kama vile ‘’email’’ au ‘’telex’’.

---

[39] Sehemu ya Utangulizi ya Mwongozo wa Kisheria wa Tume ya Kimataifa ya Biashara chini ya Umoja wa Mataifa (UNCITRAL Model Law on International Commercial Arbitration 1985) inashauri nchi zote kuzingatia Mwongozo huo wa sharia.ili kuweka usawa wa sharia hizo za nchi mbali mbali.
[40] The Threats and Challenges Facing Alternative Dispute Resolution in Africa – The Arbitrator
[41] Ibara ya 1(1) ya Mwongozo wa Kisheria wa Tume ya Kimataifa ya Biashara chini ya Umoja wa Mataifa (UNCITRAL Model Law on International Commercial Arbitration 1985)
[42] Ibara ya 7.

#### 4.1.4.1 Idadi ya Wasuluhishi

Eneo jengine muhimu lililobainishwa katika Mwongozo huo wa UNCITRAL ni suala la idadi ya Wasuluhishi wa Mgogoro. Mwongozo umeweka mamlaka kwa pande zinazohusika katika mgogoro kuamua juu ya idadi ya wasuluhishi katika mgogoro baina yao.[43] Ibara hiyo pia imeeleza kuwa endapo pande zinazohusika zitakaposhindwa kukubaliana kuhusu idadi ya wasuluhishi, basi wasuluhishi watatu watatumika katika mgogoro husika. Aidha, UNCITRAL kwa kupitia Ibara hiyo, imebainisha kuwa hakuna mtu yeyote atakayezuiwa kuwa Msuluhishi, isipokuwa kama pande husika katika mgogoro zitakubaliana hivyo.

#### 4.1.4.2 Uwezekano wa Msuluhishi kutokuwa Huru au kuwa na Upendeleo

Katika kuhakikisha kuwa Usuluhishi unakuwa wa haki, UNCITRAL imeweka masharti ya kutaka Msuluhishi awe huru na asiwe na upendeleo kwa upande wowote wa mgogoro aliopendekezwa kuwa Msuluhishi. Kwa msingi huo, mtu yeyote aliyeteuliwa kuwa Msuluhishi katika mgogoro fulani, anatakiwa kubainisha mapema kadri inavyowezekana, uwezekano wake wa kutokuwa huru au kutotenda haki kwa pande zote za mgogoro huo na kuzitaarifu pande husika za mgogoro, isipokuwa kama pande hizo zilishataarifiwa kabla.[44] Aidha, pande zinazohusika zinaweza kueleza wasiwasi wa Msuluhishi kutokuwa huru, au kuonyesha upendeleo au kutokuwa na sifa zinazohitajika kwa ajili ya usuluhishi wa mgogoro wao, endapo atabaini baada ya usuluhishi kuanza na kuwa na sababu za msingi za kuamini hivyo. Suala hili linatokana na msingi mwengine uliowekwa na UNCITRAL wa kutaka

[43] Ibara ya 10.
[44] Ibara ya 12.

pande zote katika mgogoro kutendewa sawa na kupewa fursa sawa ya kuwasilisha kesi yake.[45]

#### 4.1.4.3 Uwezo wa kutoa Uamuzi wa Mpito

UNCITRAL pia imetoa uwezo kwa Msuluhishi kutoa uamuzi wa mpito, kabla ya kumaliza kusikiliza mgogoro husika.[46] Msuluhishi atatoa uamuzi huo wa mpito endapo ataombwa na moja ya wahusika wa mgogoro huo. Uamuzi huo unapaswa kulinda kitu kinachobishaniwa ikiwa kusubiri maamuzi ya mwisho kunaweza kuathiri kitu hicho au upande mmoja kati ya pande husika.

#### 4.1.4.4 Kuanza kwa Usuluhishi

UNCITRAL pia imeweka muda wa kuanza kwa usuluhishi. Kwa mujibu wa Ibara ya 21 ya Mwongozo wa UNCITRAL wa Usuluhishi wa biashara, usuluhishi wa mgogoro unaanza siku ambayo maombi ya Usuluhishi yatapokelewa na mjibu maombi (respondent). Hata hivyo, Ibara hiyo imetoa mamlaka kwa pande zinazohusika na mgogoro, kutofautiana na msimamo huo, na hivyo kuweka muda mwengine wa kuanza kwa usuluhishi.

### 4.1.5 Mkataba uliorekebishwa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi wa 1993

Mkataba wa Jumuiya ya Kiuchumi wa Nchi za Afrika Magharibi ni makubaliano jumuishi yaliyosainiwa na nchi wanachama zinazounda Jumuiya ya Kiuchumi ya

[45] Ibara ya 18.
[46] Ibara ya 17.

Nchi za Afrika Magharibi. Mkataba wa awali ulitiwa saini na wakuu wa nchi na serikali wa nchi wanachama 16, mnamo mwaka 1975 huko Lagos, Nigeria. Pamoja na maendeleo mapya na mamlaka ya Jumuiya, Mkataba uliorekebishwa ulitiwa saini huko Cotonou, Jamhuri ya Benin mnamo mwaka 1993 na wakuu wa nchi na serikali za nchi wanachama 15.[47]

Umuhimu wa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro umeelezwa katika Mkataba uliorekebishwa wa Jumuiya ya Nchi za Afrika Magharibi. Miongoni mwa masharti ya makubaliano ya Mkataba huo kuhusiana na utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluishi ni kwamba mgogoro wowote kuhusiana na tafsiri au matumizi ya masharti ya Mkataba huu, utasuluhishwa kirafiki kwa njia ya makubaliano ya moja kwa moja bila ya upendeleo kwa masharti ya Mkataba huu na Itifaki husika.[48]

### 4.1.6 Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wa 1999

Jumuiya ya Afrika Mashariki ni jumuiya ya kikanda ya kiserikali ya nchi washirika saba yenye makao makuu yake Arusha, Tanzania, ikijumuisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Burundi, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Jamhuri ya Uganda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.[49] Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulitiwa saini tarehe 30 Novemba 1999 na kuanza kutumika tarehe 7 Julai 2000 kufuatia kuridhiwa kwake na nchi washirika tatu za awali ikiwemo Kenya, Uganda na Tanzania. Jamhuri ya Rwanda

---

[47] https://ecowas.int/ecowas-law/treaties/

[48] Ibara ya 76(1) ya Mkataba uliorekebishwa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi.

[49] https://www.eac.int/overview-of-eac#:~:text=The%20East%20African%20Community%20(EAC,its%20headquarters%20in%20Arusha%2C%20Tanzania.

na Jamhuri ya Burundi zilikubali Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 18 Juni 2007 na kuwa wanachama kamili kuanzia tarehe 1 Julai 2007.[50]

Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeweka masharti ya kuzingatiwa katika utumiaji wa njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika masuala ya usuluhishi na makubaliano. Mkataba huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeeleza kama ifuatavyo:[51]

Mahkama itakuwa na uwezo wa kusikiliza na kuamua shauri lolote:

a) linalotokana na kifungu cha usuluhishi kilichomo kwenye mkataba au makubaliano ambayo yanatoa mamlaka ambayo Jumuiya au taasisi yake yoyote ni mwanachama;

b) linatokana na mgogoro kati ya nchi wanachama kuhusu Mkataba huu ikiwa mgogoro unawasilishwa kwake chini ya makubaliano maalum kati ya nchi washirika zinazohusika; au

c) linatokana na kifungu cha usuluhishi kilichomo katika mkataba wa kibiashara au makubaliano ambayo wahusika wametoa mamlaka kwa Mahkama.

### 4.1.7 Sera ya Uwekezaji ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi ya 2018

Sera ya Uwekezaji ya ECOWAS ni miongoni mwa miongozo muhimu ambayo hutoa dira na mwelekeo wa kimaendeleo wa nchi za magharibi mwa Afrika. Pamoja na miongozo na mipango ya kimaendeleo iliyomo katika sera hiyo, Sera ya ECOWAS imetambua umuhimu wa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro

[50] https://www.mea.gov.in/Portal/ForeignRelation/east-african-community-april-2011.pdf

[51] Ibara ya 32, Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa 1999.

katika nyanja za uwekezaji, uchumi na biashara kwa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo. Sera hiyo imeeleza kuwa uwezo wa kutatua migogoro ya kibiashara hasa migogoro inayohusisha uwekezaji, haki za mali binafsi au ukiukaji wa mikataba, ni hitaji la msingi kwa ajili ya masoko kutumika ipasavyo. Kwa serikali kuboresha utawala wa sheria kunajumuisha chaguzi za utatuzi wa migogoro nchini, hasa kupitia mazungumzo ya wahusika binafsi, mashauriano, upatanishi, mifumo ya malalamiko ya wawekezaji na njia nyengine mbadala za utatuzi wa migogoro ya nchi zinazowekeza, ikijumuisha usuluhishi wa kimataifa.[52]

Aidha, Sera hii imeeleza kuwa mbinu bora za utatuzi wa migogoro huongeza utabiri katika mahusiano ya kibiashara kwa kuwahakikishia wawekezaji wa kitaifa, kikanda au nje ya kanda, kwamba haki zao za kisheria zitalindwa ipasavyo na Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro au mapitio ya Mahkama. Ikiwa taratibu za kutatua migogoro zina urasimu kupita kiasi au zinakuwa ngumu kutekelezwa, au migogoro inashindwa kutatuliwa kwa wakati na kwa gharama nafuu, makampuni yanaweza kuzuia shughuli zao za uwekezaji katika nchi husika.[53]

### 4.1.8 Shirika la Kimataifa la Hakimiliki (WIPO)

Jukumu la WIPO katika kutekeleza ulinzi wa hakimiliki, liliongezeka katikati ya miaka ya 1990, ilipotia saini makubalino ya ushirikiano na Shirika la Biashara

[52] Sera ya Uwekezaji ya ECOWAS, Sura ya 15(1)(a)(1).
[53] Sera ya Uwekezaji ya ECOWAS, Sura ya 15(1)(a)(2).

Ulimwenguni. Biashara ya kielektroniki ilipozidi kukuwa kupitia maendeleo ya mtandao, WIPO ilipewa jukumu la kusaidia kutatua migogoro kuhusu matumizi ya majina ya vikoa vya mtandao (internet domain names).[54]

Shirika la Kimataifa la Hakimiliki kupitia Kanuni zake za kusaidia kutatua migogoro, limeweka taratibu za kufuatwa katika kutatua migogoro mbali mbali ya kibiashara. Miongoni mwa taratibu hizo ni kama ifuatavyo:

**a) Uwasilishaji wa Ombi la Upatanishi**

Shirika hilo la Kimataifa limeeleza kuwa muhusika katika Makubaliano ya Upatanishi anayetaka kuanzisha Upatanishi, atawasilisha kwa maandishi Ombi la Upatanishi kwa Kituo na kwa upande mwengine wa mgogoro. Ombi la Upatanishi litawasilishwa kwa baruapepe au njia nyenginezo za mawasiliano ya kielektroniki ambazo zinatoa rikodi, isipokuwa kama muhusika ataamua kutumia huduma ya posta au huduma ya barua iliyoharakishwa.[55]

Aidha, Kanuni zimeeleza kuwa Ombi la Upatanishi litajumuisha au kuambatana na:[56]

i) majina, anuani na simu, baruapepe na taarifa nyengine za mawasiliano ya wahusika kwenye mgogoro na mwakilishi wa muhusika anayewasilisha Ombi la Upatanishi;

ii) nakala ya Makubaliano ya Upatanishi; na

iii) maelezo mafupi ya mgogoro.

[54] https://en.wikipedia.org/wiki/World_Intellectual_Property_Organization
[55] ibara ya 3(a), Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki.
[56] ibara ya 3(b), Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki.

Vile vile, Kanuni za WIPO zimeeleza kuwa Kituo kitatoa taarifa mara moja kwa wahusika kwa maandishi kuhusu kupokelewa kwa Ombi la Upatanishi na tarehe ya kuanza kwa Upatanishi huo.[57]

**b) Uteuzi wa Wapatanishi**

**a.** Kanuni hizi zimeeleza kuwa isipokuwa wahusika wenyewe wamekubaliana vyenginevyo juu ya mtu ambaye atakuwa Mpatanishi au kwa utaratibu mwengine wa kumteua Mpatanishi, uteuzi huo utafanyika kwa utaratibu ufuatao:[58]

i) Kituo kitatuma kwa kila muhusika orodha iliyo sawa ya Wapatanishi wanaopendekezwa. Orodha hiyo kwa kawaida hujumuisha majina ya Wapatanishi wasiopungua watatu kwa mpangilio wa kialfabeti. Orodha hiyo itajumuisha au kuambatana na maelezo ya sifa za kila Mpatanishi. Ikiwa wahusika wamekubaliana juu ya sifa fulani, orodha itakuwa na majina ya Wapatanishi wanaokidhi sifa hizo;

ii) Kila muhusika atakuwa na haki ya kufuta majina ya Wapatanishi au Mpatanishi yeyote ambaye uteuzi wake anaupinga na kuweka idadi ya Wapatanishi waliobaki ambao anapendelea;

iii) Kila muhusika atarejesha Kituoni orodha iliyotiwa alama ndani ya siku saba baada ya tarehe ambayo orodha hiyo inapokelewa. Muhusika yeyote atakaeshindwa kurejesha orodha iliyowekwa alama ndani ya muda uliotajwa, itachukuliwa kuwa amekubaliana na wagombea wote wanaoonekana katika orodha hiyo;

---

[57] ibara ya 6, Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki

[58] ibara ya 7(a), Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki

iv) Haraka iwezekanavyo baada ya kupokea orodha kutoka kwa wahusika, au kushindwa, baada ya kumalizika kwa muda ulioainishwa katika aya ndogo iliyotangulia, Kituo kitateua mtu kuwa Mpatanishi kutoka kwenye orodha kwa kuzingatia matakwa na pingamizi zilizooneshwa;

v) Ikiwa orodha ambazo zimerejeshwa hazioneshi mtu ambae amekubalika kwa wahusika wote kama ni Mpatanishi, Kituo kitaidhinisha kuteua Mpatanishi. Kituo vile vile kitakuwa na mamlaka ya kufanya hivyo ikiwa mtu hawezi au hataki kukubali mwaliko wa Kituo kuwa Mpatanishi, au ikiwa kunaonekana kuwa na sababu nyengine zinazomzuia mtu huyo kuwa Mpatanishi, au hakuna mtu aliyebaki ambae atakubalika kwa wahusika kuwa Mpatanishi.

**b.** Aidha, Kanuni hizi zimeeleza kuwa, bila kujali utaratibu uliowekwa katika aya ya (a), Kituo kitakuwa na mamlaka ya kumteua Mpatanishi ikiwa itaona kuwa utaratibu uliowekwa haufai kwa shauri husika;[59]

**c) Uwakilishaji wa Wahusika wa Mgogoro na Ushiriki katika vikao vya Upatanishi**

Kanuni za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki limeruhusu suala zima la kumuwakilisha muhusika wa mgogoro katika Upatanishi. Kanuni imeeleza, wahusika wanaweza kuwakilishwa au kusaidiwa wakati wa kukutana na Mpatanishi.[60]

---

[59] ibara ya 7(b), Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki.

[60] ibara ya 9(a), Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki.

Pia, Kanuni imeendelea kueleza, mara tu baada ya kuteuliwa kwa Mpatanishi, majina na anuani za watu walioidhinishwa kumuwakilisha muhusika, na majina na nyadhifa za watu watakaohudhuria katika vikao vya kukutana na Mpatanishi kwa niaba ya muhusika, yatawasilishwa na muhusika kwenda kwa muhusika mwengine, Mpatanishi na Kituo.[61]

**d) Ada kwa Wapatanishi**

Kanuni hizi zimeeleza kuwa kiwango na fedha kwa Mpatanishi na muda wa malipo yao yatapangwa na kuwekwa na Kituo, baada ya kushauriana na Mpatanishi na wahusika wa mgogoro.[62]

Aidha, Kanuni hii imeeleza, kiwango cha ada, isipokuwa wahusika na Mpatanishi wakubaliane vyenginevyo, kitatozwa kwa misingi ya viwango vya kila siku vya saa vinavyotumika katika tarehe ya Ombi la Upatanishi, kuzingatia kiwango cha mgogoro, ugumu wa mada inayobishaniwa na hali nyengine zozote za kesi husika.[63]

**e) Mwenendo wa Upatanishi**

Shirika la Kimataifa la Hakimiliki kupitia Kanuni zake za Utatuzi wa Migogoro kwa njia ya Upatanishi, zimetoa fursa kwa wahusika kukubaliana na kuchagua njia ya kufanya Upatanishi. Kanuni imeeleza, Upatanishi utafanywa kwa njia ambayo wahusika wamekubaliana, ikijumuisha mikutano kwa njia simu, mikutano kwa njia vidio, au kutumia zana za kimtandao, na ikiwa wahusika wameshindwa kukubaliana

[61] ibara ya 9(b), Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki.
[62] ibara ya 23(a), Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki
[63] ibara ya 23(b), Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki

juu ya namna ambayo Upatanishi utafanyika, Mpatanishi, kwa mujibu wa Kanuni hizi, ataamua namna ya kufanyika kwa Upatanishi huo.[64]

**f) Uwasilishaji wa Ombi na kuanza kwa Usuluhishi**

Kwa mujibu wa Kanuni za Usuluhishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki, Usuluhishi unaanza kwa uwasilishaji wa Ombi la Usuluhishi kwa Kituo cha Usuluhishi na vile vile ombi hilo kupelekwa kwa mlalamikiwa. Kanuni hizi zimeeleza, mlalamikaji atapeleka Ombi la Usuluhishi kwa Kituo na kwa mlalamikiwa.[65]Pia Kanuni hii imeeleza kuwa tarehe ya kuanza kwa Usuluhishi itakuwa tarehe ambayo Ombi la Usuluhishi limepokelewa na Kituo.[66] Ombi la Usuluhishi litajumuisha:[67]

i. madai kwamba mgogoro huo upelekwe kwenye Usuluhishi chini ya Kanuni za WIPO;
ii. majina, anuani, simu, baruapepe na namna nyengine ya mawasiliano ya wahusika wa mgogoro na ya mwakilishi wa mlalamikaji;
iii. nakala ya makubaliano ya Usuluhishi, na kifungu cha Sheria ambacho watakichagua ikiwa kitahitajika kutumika;
iv. maelezo mafupi na hali ya mgogoro, ikijumuisha viashiria vya uwepo wa mali na haki, na hali yoyote ya teknolojia inayohusika;
v. maelezo ya fidia inayoombwa na kiwango kinachodaiwa kwa kadri itakavyowezekana;

[64] ibara ya 10, Kanuni za Upatanishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki
[65] ibara ya 6, Kanuni za Usuluhishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki
[66] ibara ya 7, Kanuni za Usuluhishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki
[67] ibara ya 8, Kanuni za Usuluhishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki

vi. mapendekezo yoyote yanayohitajika, na uchunguzi wowote ambao mlalamikaji anaona ni muhimu kuhusiana na ibara ya 14 mpaka 20; na

vii. kitambulisho cha mfadhili ikiwa kitahitajika. Iwapo makubaliano ya ufadhili yatahitimishwa katika hatua ya baadae ya shauri husika, utambulisho wa mfadhili utawekwa wazi mara moja kwa wahusika, Kituo na Mahkama.

**g) Uwakilishaji katika Usuluhishi**

Kanuni za Usuluhishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki zimetambua suala la uwakilishaji wa wahusika wa mgogoro katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya Usuluhishi. Kanuni imeeleza, wahusika wanaweza kuwakilishwa na watu watakaowachagua bila kujali utaifa au sifa zao za kitaaluma. Majina, anuani na simu, baruapepe na taarifa nyengine za mawasiliano za wawakilishaji zitawasilishwa katika Kituo cha Usuluhishi na upande mwengine wa mgogoro.[68]

Aidha, Kanuni hii imeeleza kuwa kila muhusika wa mgogoro atahakikisha kuwa muwakilishi wake ana muda wa kutosha ambao utawezesha usuluhishi kumalizika kwa haraka, wahusika pia wanaweza kusaidiwa na watu watakaowachagua.[69]

### 4.1.9 Kituo cha Kikanda cha Cairo cha Usuluhishi wa Kimataifa wa Biashara (CRCIA)

Kituo cha Kikanda cha Cairo cha Usuluhishi wa Kimataifa wa Biaishara kimeanzishwa 1979 chini ya mwamvuli wa Shirika la Ushauri wa Kisheria la Afrika na Asia (AALCO), kufuatia uamuzi wa AALCO uliofikiwa katika Mkutano wa

[68] ibara ya 13(a), Kanuni za Usuluhishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki
[69] ibara ya 13(a)(b), Kanuni za Usuluhishi za Shirika la Kimataifa la Hakimiliki

Doha wa 1978 wa kuanzisha vituo vya kikanda vya usuluhishi wa kimataifa wa biashara. Kituo hiki cha kikanda kimeweka Kanuni mbali mbali ambazo hutumika kutatua migogoro katika maeneo mbali mbali kama ifuatavyo:

**a) Wataalamu kuteuliwa na Kituo ya Usuluhishi**

Kanuni za Kituo hiki zimeeleza, baada ya kushauriana na wahusika wa mgogoro, mahkama ya usuluhishi inaweza kuteua mtaalamu huru mmoja au zaidi kuwasilisha mahkamani kwa maandishi, juu ya masuala maalum ya kuamuliwa na mahkama. Nakla ya hadidu rejea zilizoandaliwa na mahkama ya usuluhishi zitawasilishwa kwa wahusika wa mgogoro.[70]

**b) Kuchagua kanuni za sheria zitakazotumika katika Usuluhishi wa Kimataifa**

Kwa mujibu wa Kanuni za Kituo cha Kikanda cha Cairo cha Usuluhishi wa Kimataifa wa Biashara, kanuni za sheria ambazo zitatumika ni zile kanuni za sheria ambazo zimechaguliwa na wahusika kutumika katika suala la mgogoro husika. Ikiwa wahusika watashindwa kuchagua kanuni zitakazotumika katika mgogoro wao, mahkama ya usuluhishi itatumia sheria ambayo ina uhusiano wa karibu na mgogoro huo.[71]

**c) Marekebisho ya madai au utetezi**

Kanuni za Kituo cha Kikanda cha Cairo cha Usuluhishi wa Kimataifa wa Biashara kimetoa fursa kwa wahusika wa mgogoro kufanya marekebisho katika madai au

[70] ibara ya 29(1), Kanuni za Kituo cha Kikanda cha Cairo cha Usuluhishi wa Kimatifa wa Biashara
[71] ibara ya 35, Kanuni za Kituo cha Kikanda cha Cairo cha Usuluhishi wa Kimataifa wa Biashara

utetezi wao. Kanuni imeeleza, wakati wa Usuluhishi mhusika anaweza kurekebisha madai yake, utetezi, madai ya kupinga au madai ya madhumuni ya kufutwa, isipokuwa Kituo cha Usuluhishi kikiona kuwa kufanya marekebisho hayo kutasababisha kuchelewa au itamuathiri muhusika mwengine au hali ya dai husika. Hata hivyo, madai, utetezi, madai ya kupinga au madai ya madhumuni ya kufutwa, hayawezi kurekebishwa ikiwa dai au utetezi uliorekebishwa upo nje ya mamlaka ya mahkama ya usuluhishi.[72]

## 4.2 SHERIA NA UZOEFU WA NCHI MBALI MBALI

### 4.2.1 Jamhuri ya Kenya

#### 4.2.1.1 Sheria ya Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 26 ya 2013.

**a) Kuanzishwa kwa Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa**

Miongoni mwa hatua kubwa za utatuzi wa migogoro ambazo zimechukuliwa na Serikali ya Kenya ni pamoja na kuanzisha Sheria maalum ya Kituo cha Usuluhishi wa Kimataifa. Kwa mujibu wa Sheria hii, Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa ni chombo kinachojitegemea chenye uwezo wa kurithi na kurithiwa, na kina muhuri wake, na kwa kutumia jina lake, kina uwezo wa kushtaki na kushtakiwa, kuchukua, kununua au vyenginevyo kujipatia, kuzuia, kutoza au kuondosha mali inayohamishika au isiyohamishika; kukopa fedha; na kufanya au kutekeleza mambo mengine yoyote kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii

[72] ibara ya 22, Kanuni za Kituo cha Kikanda cha Cairo cha Usuluhishi wa Kimataifa wa Biashara

ambayo yanaweza kisheria kufanywa au kutekelelezwa na chombo kinachojitegemea.[73] Kituo hiki kina majukumu yafuatayo:[74]

i. kukuza, kuwezesha, kuhimiza mwenendo wa usuluhishi wa kimataifa wa kibiashara kwa mujibu wa Sheria hii;
ii. kusimamia usuluhishi wa ndani na wa kimataifa pamoja na mbinu za utatuzi mbadala wa migogoro chini ya mwamvuli wake;
iii. kuandaa sheria zinazojumuisha michakato ya upatanishi;
iv. kuandaa makongamano ya kimataifa, semina na mafunzo kwa wasuluhishi na wanazuoni;
v. kudumisha ushirikiano na taasisi nyengine za kikanda na kimataifa katika maeneo muhimu katika kufikia malengo ya Kituo;
vi. kutoa msaada na ushauri kwa ajili ya kutafsiri na kutekeleza tunzo za usuluhishi;
vii. kuzuia, kusimamia na kutumia Mfuko kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;
viii. kutoa ushauri wa kiufundi na kiutaratibu kwa wahusika wa mgogoro;
ix. kutoa mafunzo na vibali kwa wasuluhishi na wapatanishi; n.k.

**b) Kuanzishwa kwa Mahkama ya Usuluhishi**

Sheria ya Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa imeanzisha mahkama ambayo hujulikana kama Mahkama ya Usuluhishi. Mahkama hii imeundwa na Rais, Manaibu Rais wawili, wajumbe wengine kumi na tano ambao wote watakuwa wasuluhishi wa kimataifa, na Mrajis.[75] Aidha Mahkama hii ina mamlaka ya awali

[73] kifungu cha 4(1)(2), Sheria ya Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 26 ya 2013.
[74] kifungu cha 5, Sheria ya Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 26 ya 2013.
[75] kifungu cha 21(1)(2), Sheria ya Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 26 ya 2013.

na rufaa ya kusikiliza na kuamua mizozo ambayo huwasilishwa kwake kwa mujibu wa Sheria hii na sheria nyengine na maamuzi yanayotolewa na Mahkama hii ni ya mwisho.[76]

### 4.2.2 Uzoefu wa Tanzania Bara

#### 4.2.2.1 Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Bara Nam. 2 ya 2020

**a) Kuanzishwa kwa Kituo cha Usuluhishi cha Tanzania Bara**

Sheria ya Usuluhishi Tanzania Bara imeanzisha kituo maalum cha utatuzi wa migogoro ambacho hujulikana kama Kituo cha Usuluhishi cha Tanzania Bara. Kituo hiki cha Usuluhishi cha Tanzania Bara kinaongozwa na kusimamiwa na Bodi ya Uongozi ambayo itakuwa na wajumbe watakaoteuliwa kwa mujibu wa sifa maalum, na Sheria imebainisha muda wa kutumikia ofisi, muda wa kufanya mikutano hatua za kinidhamu kwa wajumbe wa Bodi n.k.[77]

**b) Kuainishwa kwa wajibu wa Baraza la Usuluhishi**

Chini ya Sheria hii ya Usuluhishi ya Tanzania Bara, kumeainishwa wajibu wa Baraza la Usuluhishi ambao kimsingi unatakiwa kutekelezwa wakati wa kusuluhisha migogoro mbali mbali inayowasilishwa Barazani hapo. Miongoni mwa wajibu huo ni pamoja na kutenda haki na bila kufanya upendeleo kwa wahusika wa mgogoro, kumpa kila muhusika fursa ya kutosha ya kujenga kesi yake dhidi ya mpinzani wake,

---

[76] kifungu cha 22(1)(2), Sheria ya Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 26 ya 2013.
[77] kifungu cha 77(1)(4), Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Bara Nam. 2 ya 2020.

kutumia taratibu ambazo zitafaa kwa mujibu wa hali ya kesi ilivyo, kujiepusha na ucheleweshaji na gharama zisizokuwa za lazima ili kutoa njia bora na za haki kwa utatuzi bora wa migogoro. Baraza litatekeleza wajibu huo katika kufanya usuluhishi, katika kutoa maamuzi juu ya taratibu na ushahidi na katika kutekeleza mamlaka yote iliyopewa.[78]

**c) Kupewa uwezo Baraza la Usuluhishi kutoa tunzo kwa maswala tofauti yanayobishaniwa**

Baraza la Usuluhisi limepewa uwezo na Sheria ya Usuluhisi ya Tanzania kutoa tunzo kwa nyakati tofauti kwa mujibu wa vipengele vinavyobishaniwa katika mgogoro uliowasilishwa. Sheria hii imeeleza kuwa isipokuwa kama wahusika wa mgogoro wamekubaliana vyenginevyo, Baraza la Usuluhishi litatoa tunzo zaidi ya moja katika nyakati tofauti juu ya vipengele tofauti kwa mujibu wa jambo ambalo linatafutiwa ufumbuzi. Katika kutekeleza swala hili, Baraza la Usuluhishi linaweza kutoa tunzo juu ya mambo ambayo yanaathiri dai zima au sehemu ya dai lililowasilishwa.[79]

**d) Tunzo kusimamiwa kama ni hukmu au amri ya Mahkama**

Pale ambapo wahusika wa mgogoro hupeleka madai yao mbele ya Msuluhishi kwa ajili ya kusuluhishwa, tunzo inayotolewa na kusainiwa na pande zote za mgogoro, kwa ruhusa ya Mahkama, husimamiwa kama ni hukumu au amri ya Mahkama. Sheria hii imeeleza wazi kuwa tunzo inayotolewa na Baraza la usuluhishi kutokana

[78] kifungu cha 35(1)(2), Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Bara Nam. 2 ya 2020.
[79] kifungu cha 49(1)(2).

na makubaliano ya usuluhishi, kwa ruhusa ya Mahkama, inaweza kusimamiwa kwa namna ile ile kama ni hukumu au amri ya Mahkama.[80]

**e) Kituo kusajili wasuluhishi**

Ili wasuluhishi wa migogoro watambulike kisheria, ni lazima wasajiliwe na majina yao kuwekwa katika orodha maalum. Miongoni mwa kazi za msingi za Kituo cha Usuluhishi cha Tanzania Bara ni pamoja na kufanya usajili wa wasuluhishi wa migogoro. Kituo hicho husajili na kutunza orodha wa wasuluhishi wote walioidhinishwa.[81]

**f) Uwezo wa Kituo cha Usuluhishi kumuondoa Msuluhishi**

Kituo cha Usuluhishi wa migogoro Tanzania Bara kimepewa uwezo wa kumuondoa Msuluhishi chini ya Sheria hii. Muhusika katika usuluhishi, baada ya kutoa taarifa kwa muhusika wa pili, Msuluhishi wa mgogoro wao na msuluhishi mwengine, anaweza kuomba Kituo cha Usuluhishi kumuondoa Msuluhishi aliyekuwa akisimamia mgogoro wao kutokana na yoyote kati ya sababu zifuatazo:[82]

i. ikiwa msuluhishi ataonesha kuwa na upendeleo.
ii. ikiwa msuluhishi hana sifa inayohitajika kwa mujibu wa makubaliano ya usuluhishi;
iii. ikiwa msuluhishi hana uwezo kimwili au kiakili kuendesha usuluhishi au kuna mashaka juu ya uwezo wake wa kuendesha usuluhishi;

[80] kifungu cha 68(1).
[81] kifungucha 77(3)(b), Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Bara Nam. 2 ya 2020.
[82] kifungu cha 26(1), Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Bara Nam. 2 ya 2020.

iv. ikiwa msuluhishi amekataa au ameshindwa kuendesha usuluhishi, kutumia uwezo na njia imara za kufanya usuluhishi, kutoa tunzo na dhuluma kubwa imesababishwa au itasababishwa na muombaji.

Msuluhishi ambaye maombi ya kumuondoa yamefanywa dhidi yake, atakuwa na haki ya kusikilizwa kabla ya Kituo.[83]

### 4.2.3 Uzoefu wa nchi ya Ghana

**4.2.3.1 Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ya** Usuluhishi kutoa amri chini ya

**2010**

Kwa kuzingatia umuhimu wa kutatua migogoro mbali mbali inayoibuka miongoni mwa watu wa Ghana, Bunge la Jamhuri ya nchi hiyo limetunga sheria yenye kutoa miongozo na kubainisha taratibu sahihi za kufuatwa na wananchi pale ambapo kwa hiyari yao wameamua kutatua migogoro yao kwa utaratibu usiokuwa wa Mahkama na wenye kutambulika kisheria. Sheria hiyo hujulikana kama Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ya 2010. Maeneo mengi ya msingi ya kuzingatiwa yametajwa na kufafanuliwa katika Sheria hii. Miongoni mwa maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

#### a) Ada kwa Wasuluhishi

Katika kutekeleza majukumu yao ya kutatua migogoro iliyoletwa mbele yao na wahusika wa migogoro hiyo, Wasuluhishi wanatakiwa kulipwa fedha kama ni ada ya usuluhushi. Ada hiyo hulipwa kutokana na makubaliano baina ya wahusika wa

[83] kifungu cha 26(5), Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Nam. 2 ya 2020.

mgogoro na Msuluhishi, na wahusika kwa kushirikiana na kwa mmoja mmoja, watawajibika kulipa fedha ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa makubaliano. Hii inathibiti pale Sheria hii ilipoeleza kuwa wahusika na wasuluhishi watakubaliana juu ya ada itakayolipwa na wahusika kwa mujibu wa usuluhishi na wahusika kwa kushirikiana na kwa mmoja mmoja kufanya malipo ya ada hiyo waliyokubaliana na ukitokezea mgogoro kuhusiana na ada, basi muhusika anaweza kupeleka suala hilo katika mamlaka iliyoteua msuluhishi au Mahkamani kwa ajili ya kuutatua.[84]

Kwa mujibu wa Sheria hii, ada italipwa kwa mujibu wa thamani ya shauri la usuluhishi, ugumu wa kesi husika na kiwango cha ada kilichokubaliwa kwa saa.[85]

**b) Kinga kwa Wasuluhishi**

Sheria hii pia imeweka kinga kwa wasuluhishi wa migogoro kuwa wakati wa kutekeleza majukumu yao, hawatowajibika kwa kitendo chochote walichokifanya au kuacha kufanya kwa sharti kwamba utekelezaji huo wa majukumu umefanywa kwa nia safi.[86]

**c) Uwezo wa Msuluhishi kuteua mtaalamu**

Katika maeneo ambayo yanahitaji utaalamu wakati wa usuluhishi, Sheria hii imempa uwezo Msuluhishi kuteua mtu yeyote ambaye ataona utaalamau wake unafaa katika kusaidia kuleta suluhu juu ya mgogoro uliopo mbele yake. Katika kufanya uteuzi huo, Msuluhishi atatakiwa kuwasiliana na wahusika wa mgogoro

[84] kifungu cha 22(1), Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ya Ghana ya 2010.
[85] kifungu cha 22(2).
[86] kifungu cha 23(1), Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ya Ghana ya 2010.

huo.[87] Wahusika nao watatakiwa kuwasilisha taarifa sahihi na kutoa waraka wowote ambao mtaalamu atahitaji kwa ajili ya uchunguzi.[88]

**d) Kuanzishwa kwa Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro**

Katika kutatua na kusimamia ipasavyo migogoro ya wananchi wa nchini Ghana, Sheria hii imeanzisha kituo maalum kinachojulikana kama ni Kituo cha Njia mbadala za Utatuzi wa Migogoro.[89] Lengo la msingi la kituo hiki ni kuwezesha shughuli zote za utatuzi mbadala wa migogoro.[90] Katika kufikia lengo hilo, kituo hicho kitatekeleza majukumu yafuatayo:[91]

(a) kutoa nyenzo za utatuzi wa migogoro kupitia usuluhishi, upatanishi na taratibu nyengine za utatuzi wa migogoro;

(b) kusajili wasuluhishi na wapatanishi;

(c) kutoa orodha ya wasuluhishi na wapatanishi kwa watu ambao wataomba huduma ya msuluhishi na mpatanishi;

(d) kutoa miongozo ya ada kwa wasuluhishi na wapatanishi

(e) kupanga utoaji wa msaada kwa watu pale itakapohitajika;

(f) kuchunguza Kanuni za usuluhishi na upatanishi chini ya Sheria hii na kupendekeza mabadiliko katika Kanuni;

(g) kufanya tafiti, kutoa elimu na kutoa machapisho juu ya aina zote za njia mbadala za utatuzi wa migogoro;

[87] kifungu cha 43(1).
[88] kifungu cha 43(2).
[89] kifungu cha 114(1).
[90] kifungu cha 115(1).
[91] kifungu cha 115(2).

(h) kuweka ofisi za Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro katika ngazi za Mikoa na Wilaya kama ambavyo Bodi itaona inafaa; n.k

Aidha, Sheria hii imeeleza kuwa kwa mujibu wa Katiba na pale itakavyoelezwa vyenginevyo katika Sheria hii au sheria nyengine, Kituo hakitokuwa chini ya maelekezo au udhibiti wa mtu yeyote au mamlaka yoyote katika kutekeleza majukumu yake.[92] Pia Sheria hii imeeleza kuwa Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro kitaongozwa na Bodi.[93]

**e) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro**

Sheria hii pia imeanzisha Mfuko ambao hujulikana kama ni Mfuko wa Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ambao vyanzo vyake vya fedha ni pamoja na ruzuku kutoka Serikalini ambayo hutolewa kwa ajili ya maendeleo ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro, tozo na ada zinazotozwa na Kituo katika kutekeleza majukumu yake na michango na zawadi kutoka kwa umma, taasisi na jumuiya.[94]

### 4.2.4 Uzoefu wa nchi ya Mauritius

#### 4.2.4.1 Sheria ya Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 37 ya 2008

**a) Kuwakilishwa kwa muhusika katika usuluhishi endapo atafariki, kufilisika au kumalizika kwake (winding up)**

Sheria hii ya nchini Mauritius imetambua umuhimu wa kuendelea na taratibu na hatua za usuluhishi hata katika mazingira ambayo muhusika wa mgogoro amefariki,

[92] kifungu cha 116.
[93] kifungu cha 117.
[94] kifungu cha 125(1),(2).

amefilisika au kumalizika kwake (winding up). Katika kuendelea na mchakato wa usuluhishi, Sheria hii imetoa mamlaka kwa wawakilishi wa wahusika hao kuendelea na taratibu zote hatua kwa hatua mpaka kumalizika kwa usuluhishi na kutolewa tunzo. Kwa muktadha huo, Sheria inaeleza kuwa isipokuwa kama itakubaliwa vyenginenyo na wahusika, makubaliano ya usuluhishi hayatomalizika kwa kifo cha muhusika, kufilisika au kumalizika kwa muhusika (winding up) na kinaweza kusimamiwa na mwakilishi wa muhusika.[95]

**b) Mahkama kutoa msaada katika kuchukua ushahidi**

Sheria hiyo ya Mauritius pia imefafanua kuwa Baraza la Usuluhishi au muhusika baada ya kupata idhini kutoka kwa Baraza, anaweza kuiomba Mahkama ya Juu kusaidia katika kuchukua ushahidi. Katika kufanikisha suala hili, Mahkama itatoa wito kwa mtu yeyote kuhudhuria mbele ya Baraza la Usuluhishi kutoa ushahidi au kuwasilisha nyaraka au kitu chengine chochote. Aidha, Mahkama hiyo inaweza kumuamuru shahidi yeyote kuwasili kwa ajili ya kuulizwa maswali baada ya kulishwa kiapo mbele ya Baraza la Usuluhishi, au mbele ya Afisa wa Mahkama au mtu mwengine kwa ajili ya kutumika na Baraza la Usuluhishi.[96]

### 4.2.5 Uzoefu wa nchi ya Samoa

**Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Nam. 30 ya 2007**

**a) Kuanzishwa kwa Baraza la Upatanishi**

Katika kuhakikisha utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala pamoja na taratibu zake unasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo, Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa

[95] kifungu cha 3(1), Sheria ya Kimataifa ya Usuluhishi ya Mauritus Nam 37 ya 2008.
[96] kifungu cha 25(1)(2), Sheria ya Kimataifa ya Usuluhishi ya Mauritius Nam. 37 ya 2008.

Migogoro nchini Samoa imeanzisha chombo cha kusimamia migogoro hiyo kiitwacho Baraza la Upatanishi (Mediation Council). Baraza hili limeundwa na wajumbe wafuatao:[97]

i. Jaji Mkuu ambaye ni Mwenyekiti;
ii. Rais wa Chama cha Wanasheria au Mteule wake;
iii. Mwanasheria Mkuu au Mteule wake;
iv. Mchunguzi au Mteule wake;
v. Afisa Mtendaji Mkuu wa Wizara au Mteule wake;
vi. Rais wa Wapatanishi walioidhinishwa wa Jumuiya ya Samoa au Mteule wake;
vii. Rais wa Jumuiya ya Biashara au Mteule wake;
viii. Mjumbe aliyeteuliwa na Jaji Mkuu kwa kushauriana na Wajumbe wengine wa Baraza.

**b) Mahkama kuombwa kutoa maelekezo**

Chini ya Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ya nchini Samoa, wahusika wa mgogoro au Mpatanishi, wamepewa fursa ya kufanya maombi kwa Mahkama ili kupatiwa maelekezo. Mara tu baada ya kuanza kwa Upatanishi, Mpatanishi au muhusika katika upatanishi anaweza kufanya maombi hayo kuhusiana na masuala ya shauri katika Upatanishi.[98]

### 4.2.6 Uzoefu wa Nchi ya Ufaransa

#### 4.2.6.1 Mahkama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya nchini Ufaransa

[97] kifungu cha 6A(1), Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Nam. 30 ya 2007 ya Samoa.
[98] kifungu cha 11A, Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Nam. 30 ya 2007 ya Samoa.

Hii ni Taasisi isiyo ya faida (non-profit institution) yenye utaalamu mkubwa na toshelevu ambayo ipo kwa ajili ya kutatua migogoro ya kampuni kubwa na kampuni ndogo ndogo kwa njia ya usuluhishi na upatanishi. Mahkama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya nchini Ufaransa imehusishwa na sekta ya biashara ya nafaka na tangu wakati huo, Mahkama hiyo imepanua utaalamu wake katika sekta nyengine za viwanda na biashara. Kwa hivi sasa, utaalamu wa Mahkama ya Usuluhishi ya Ufaransa ni mkubwa na umejikita katika maeneo mengi na una mamlaka ya kuingilia aina zote za migogoro ya kiuchumi.[99]

Kwa sasa Kituo hiki kimekuwa ni kituo kikongwe katika shughuli za usuluhishi nchini Ufaransa na ndio kituo cha kwanza barani Ulaya kwa kiwango cha takwimu. Zaidi ya migogoro 40,000 inayohusiana na shughuli za kibiashara na kiviwanda imetatuliwa na Kituo hiki, na kufanya Kituo hiki kuwa na hadhi ya kimataifa. Baadhi ya mifumo ya utendaji wa Kituo hiki ni kama ifuatavyo:[100]

**a) Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya Ufaransa kuendeshwa na Bodi**

Mahkama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya nchini Ufaransa inaendeshwa na Bodi ya wakurugenzi inayojumumuisha wawakilishi wa mashirika na jumuiya za kitaaluma wenye nia ya kulinda njia bora zaidi za ushindani wa makampuni ya kibiashara na kiviwanda.

**b) Utoaji wa mafunzo maalum**

---

99 https://www.arbitrage.org/caip/?lang=en

100 https://www.arbitrage.org/caip/?lang=en

Mahkama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya nchini Ufaransa hutoa mafunzo maalum kwa wajumbe wake, washirika, watendaji mbali mbali wa biashara na kwa mtu yeyote yule ambaye anataka kufahamu zaidi masuala ya usuluhishi na upatanishi. Kituo hicho hutoa mafunzo hayo katika maana pana zaidi kwa lengo la kuwajengea uwezo na uelewa watu hao.

**c) Kuandaa warsha, matukio na semina mbali mbali**

Aidha, Mahkama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya nchini Ufaransa huandaa warsha, matukio na semina mbali mbali kwa lengo la kukuza maelewano katika kutatua migogoro kwa njia ya amani. Lengo hasa kwa makampuni ambayo yamejikita katika kulenga shughuli zao kuu na kutunza uhusiano baina yao na washirika wao, hata katika mazingira magumu.

**d) Utatuzi wa migogoro ya kimataifa**

Mashauri yanayoletwa mbele ya Mahkama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya nchini Ufaransa yana hadhi ya kimataifa kwa zaidi ya nusu ya mashauri hayo. Asilimia sabiini ya uendeshaji wa usuluhishi mahakamani hapo inahusisha angalau muhusika mmoja wa kigeni, na asilimia thelathini ya uendeshaji wa usuluhishi katika mahkama hiyo inahusisha wahusika wawili wa kigeni.

### 4.2.7 Uzoefu wa Nchi ya Uingereza

#### 4.2.7.1 Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro cha London

Kituo hiki cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro kimeweka makaazi yake katika mji wa London nchini Uingereza. Hiki ni kituo mojawapo ya vituo bora vya

kimataifa vya utatuzi wa migogoro ulimwenguni. Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro cha London hutoa vyumba bora na vya kisasa kwa ajili ya usuluhishi, upatanishi, mafunzo na masuala mengine ya umma. Aidha, Kituo hiki hutoa vifaa bora vya usikilizaji wa mashauri na kuhudumia taasisi kuu za kimataifa za utatuzi wa migogoro.[101]

#### 4.2.7.1.1 Kituo kufanya usuluhishi kwa njia za kimtandao

Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro cha London kinafanya usuluhishi wa kisasa wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya kimtandao ili kupunguza usumbufu wa usikilizwaji wa kesi na kuweka mashauri kwa wakati uliopangwa. Bila kujali maeneo ya wahusika, wasuluhishi na washiriki wengine, wasimamizi wa usuluhishi wa njia ya kimtandao hutoa muongozo na usaidizi wa kitaalamu kabla na wakati wa usuluhishi.[102]

Mikutano ya usikilizaji wa kesi kwa ajili ya kusuluhisha, hujumisha matumizi ya mbinu za mahudhurio kwenye tovuti na mitandao ili kuhakikisha kwamba wahusika wote wanaweza kushiriki kikamilifu na kwa urahisi. Mfumo huu hutumika bila kujali wahusika wapo mahali gani. Usuluhishi kwa jia za kimtandao pia hutumika katika Kituo hiki kwa kuwaunganisha wahusika ambao wamehudhuria Kituoni hapo na wale waliopo maeneo ya mbali.[103]

---

[101] https://www.idrc.co.uk/

[102] https://www.idrc.co.uk/virtual-hybrid-hearings/

[103] Ibid

## SURA YA TANO

## 5.0 MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 5.1 MAPENDEKEZO

Kwa kuzingatia maoni ya wadau, mapitio ya rejea, mikataba ya kimataifa na uzoefu wa nchi mbali mbali, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imebaini kuwa licha ya kukuwepo kwa sheria mbali mbali hapa Zanzibar ambazo zimetambua na kueleza taratibu za njia mbadala za utatuzi wa migogoro, eneo hili bado ni dhaifu na halikidhi haja na hivyo, kuhitaji kuimarishwa. Ili kuenda sambamba na kasi ya maendeleo katika nyanja za kibiashara, kazi, uwekezaji na uchumi ikiwemo uchumi wa buluu, ni muhimu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha eneo hili la utatuzi

wa migogoro ambayo huibuka katika nyanja hizo. Hivyo, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza yafuatayo:

### 5.1.1 Mapendekezo ya Kisheria

#### 5.1.1.1 Kutungwa kwa sheria mpya itakayojulikana kama Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar (Zanzibar Alternative Dispute Resolution Act)

Kutokana na mazingira halisi ya muingiliano wa wanajamii kwa hivi sasa nchini Zanzibar, mwenendo na mwelekeo wa kiuchumi, kazi, biashara na uwekezaji nchini, ni vyema ikatungwa sheria hiyo ambayo itajikita katika kutatua migogoro mbali mbali nchini. Migogoro hiyo inayoibuka katika jamii itatuliwe kwa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro. Kutungwa kwa Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro kutasaidia wahusika wanaozozana kutatua migogoro yao chini ya maafikiano yanayotokana na makubaliano baina yao.

Madai ya wahusika hao hayatapelekwa Mahkamani kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi na chombo hicho badala yake madai hayo yatatatuliwa kwa njia za mazungumzo, upatanishi au usuluhishi. Kufanya hivyo kutasaidia kuokoa muda na gharama zinazoweza kuepukika na hatimaye haki itakayoridhiwa na wahusika wa pande zote za mgogoro kupatikana. Inapendekezwa kuwa Sheria hiyo izingatie mambo muhimu yafuatayo:

**a) Aina za utatuzi wa migogoro ambazo zitatumika chini ya Sheria hii**

Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro iorodheshe aina za utatuzi wa migogoro kama vile Mazungumzo, Upatanishi na Usuluhishi (Negotiation, Mediation and Arbitration). Vile vile Sheria iweke utaratibu ambao utatumika katika kusimamia na kuendesha shughuli zote za utatuzi wa migogoro katika aina hizo.

**b) Sifa na uteuzi wa watatuzi wa migogoro wa ndani**

Sheria ieleze namna ambavyo watatuzi wa migogoro watateuliwa pamoja na kuweka muda ambao wateule hao watatumikia ofisi. Aidha, Sheria ibainishe sifa za kuteuliwa kwa wasuluhishi au wapatanishi hao. Inapendekezwa kuwa ili mtu ateuliwe kuwa Mpatanish au Msuluhishi wa ndani, awe na sifa zifuatazo:

i. Awe Mzanzibari;
ii. Awe na angalau shahada ya kwanza au inayolingana nayo katika fani ya Utatuzi wa migogoro, Sheria, Biashara, Uhandisi, Uchumi au Ustawi wa jamii;
iii. Awe na uzoefu wa fani zilizoainishwa hapo juu angalau kwa kipindi cha miaka mitano;
iv. Awe na uelewa wa masuala ya utatuzi wa migogoro, saikolojia na ushauri; na
v. Awe anaheshimika kutokana na mwenendo wake mzuri kwa Serikali na jamii kwa ujumla.

**c) Usikilizaji wa migogoro**

Sheria iweke utaratibu maalum wa kusikiliza migogoro ambao utamtaka mtatuzi wa migogoro kufanya yafuatayo:

i. kutoa taarifa kwa wahusika juu ya tarehe ya kuanza kusikiliza madai yao;
ii. kuwataka wahusika wa mgogoro kutoa taarifa binafsi za mashahidi ambao wanakusudia kuwaita kwa ajili ya kutoa ushahidi.

**d) Sheria kusimamia migogoro baina ya watu binafsi au serikali**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza, Sheria itakayotungwa itumike kusuluhisha migogoro inayoibuka baina ya watu binafsi wao kwa wao na baina ya watu binafsi na serikali. Kwa mujibu wa Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25, Usuluhishi wa mgogoro utafanyika pale ambapo upande mmoja wa mgogoro huo ni Serikali. Hivyo, Sheria itakayotungwa ihusishe na migogoro ya watu binafsi.

**e) Lugha ya kuendesha shauri**

Msingi wa uendeshaji wa mashauri katika njia mbadala za utatuzi wa migogoro ni makubaliano baina ya wahusika wa mgogoro. Kwa msingi huo, Sheria ieleze wazi kuwa lugha ambayo itatumika katika uendeshaji wa mashauri itatokana na makubalinano ya wahusika wa mgogoro. Na ikiwa wahusika watashindwa kukubaliana juu ya lugha gani itumike katika kusikiliza dai lao, Msuluhishi atachagua lugha kwa niaba yao. Hata hivyo, inapendekezwa kuwepo kwa utaratibu wa kuweka wakalimani watakaotafsiri lugha mbali mbali pale itakapohitajika na wahusika wa mgogoro.

**f) Muda wa kusimamia mgogoro hadi kumalizika kwake**

Sheria ibainishe wazi muda ambao utatumika katika kutatua migogoro kwa mujibu wa aina ya utatuzi inayotumika. Katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya upatanishi,

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa Upatanishi usizidi miezi sita na kwa upande wa Usuluhishi, isizidi miezi kumi.

**g) Marekebisho ya madai au utetezi**

Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza, Sheria itakayotungwa iweke kifungu maalum kitakachowapa fursa wahusika wa mgogoro kufanya marekebisho ya madai yao, utetezi, madai ya kupinga au madai ya madhumuni ya kufutwa. Wahusika wa mgogoro wapewe fursa hiyo ya kisheria katika Usuluhishi (Arbitration) ikijumuisha pia Usuluhishi wa Kimataifa wa Biashara (International Commercial Arbitration). Aidha Sheria iweke kifungu kidogo kitakachompa uwezo Msuluhishi kukataa marekebisho hayo kufanyika ikiwa ataona kufanya hivyo kutasababisha kuchelewa au itamuathiri muhusika mwengine au hali ya dai husika.

**h) Kinga kwa watatuzi wa migogoro**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa moja ya masharti ya kuzingatiwa ndani ya Sheria hii ni pamoja na kuwapa kinga watatuzi wa migogoro. Inapendekezwa kuwa Sheria itambue kuwa wakati wa kutekeleza majukumu yao, watatuzi hao wa migogoro hawatowajibika kwa kitendo chochote ambacho watakifanya au wataacha kukifanya ikiwa kitendo hicho kimefanywa kwa nia safi.

**i) Uwezo wa Mahkama Kuu kuhusiana na tunzo**

Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar ieleze uwezo wa Mahkama Kuu wa kusimamia tunzo yoyote ambayo hutolewa na Msuluhishi. Tunzo hiyo inaweza kusimamiwa kama ni hukumu au amri ya Mahkama. Kwa upande wa

tunzo ya kigeni, Sheria ieleze kuwa tunzo hiyo inaweza kusimamiwa ikiwa imetolewa na chombo chenye mamlaka na kwa mujibu wa sheria za nchi ambayo tunzo hiyo imetolewa, na kwa kuzingatia mikataba ya kimataifa.

**5.1.1.2 Kuwekwa kwa kifungu makhsusi cha kuanzisha Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar**

Ili suala la utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala liweze kutekelezwa vizuri, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwekwa kwa kifungu makhsusi katika Sheria ya Njia Mbadala ya Utatuzi wa Migogoro Zanzibar cha kuanzisha Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar (Zanzibar Alternative Dispute Resolution Centre – ADR Centre). Kituo hicho kitakachoanzishwa kiwe na sifa zifuatazo:

a) kiwe chombo kinachojitegemea;

b) kiwe na uwezo wa kurithi na kurithiwa;

c) kiwe na muhuri wake;

d) kiwe na uwezo wa kumiliki, kuuza na kutoa mali;

e) kwa kutumia jina lake, kiwe na uwezo wa kushitaki na kushitakiwa;

f) kiwe na uwezo wa kukopa fedha;

g) kiwe na uwezo wa kuingia mikataba; n.k.

Aidha, inapendekezwa Kituo hicho kiongozwe na Bodi itakayokuwa chini ya uongozi wa Mwenyekiti, ambaye atakuwa ni mtu mwenye sifa za kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar ambaye atateuliwa na Rais pamoja na Wajumbe

wengine wenye sifa maalum. Inapendekezwa kuwa ili mtu aweze kuteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi, awe na sifa zifuatazo:

i. awe Mzanzibari;
ii. awe na angalau shahada ya kwanza au inayolingana nayo katika fani ya Sheria, Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro (ADR), Uhandisi,Utawala, Biashara, Uchumi na Ustawi wa Jamii kutoka katika chuo kinachotambulika;
iii. awe na uzoefu wa fani zilizoainishwa hapo juu angalau kwa kipindi cha miaka saba;
iv. awe na taaluma ya kutosha yenye kuhusiana na njia mbadala za utatuzi wa migogoro; na
v. awe na maadili mema na kuheshimika kutokana na mwenendo wake mzima kwa Serikali na jamii kwa ujumla.

Vile vile, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar kipewe uwezo kisheria kusuluhisha migogoro ya kimataifa (international arbitration). Wawekezaji mbali mbali na wafanya biashara wa kimataifa wapate fursa ya kutumia Kituo hiki katika kutatua migogoro yao. Kwa usuluhishi wa migogoro ya kimataifa, Sheria ijumuishe wasuluihishi wenye sifa za kuwa wasuluhishi wa ndani na wasuluhishi wasiokuwa wazanzibari.

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar pia inapendekeza, Sheria hiyo itakayotungwa ibainishe kazi mbali mbali za Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar, na miongoni mwa kazi za Kituo hicho zinapendekezwa kazi zifuatazo:

(a) kutoa nyenzo za utatuzi wa migogoro kupitia usuluhishi, upatanishi na taratibu nyengine za utatuzi wa migogoro;
(b) kusajili wasuluhishi na wapatanishi;
(c) kutoa orodha ya wasuluhishi na wapatanishi kwa watu ambao wataomba huduma ya msuluhishi na mpatanishi;
(d) kukuza, kuwezesha na kuhimiza mwenendo wa usuluhishi wa kimataifa wa kibiashara kwa mujibu wa Sheria hii;
(e) kusimamia usuluhishi wa ndani na wa kimataifa pamoja na mbinu za utatuzi wa migogoro;
(f) kuandaa makongamano ya kimataifa, semina na mafunzo kwa wasuluhishi;
(g) kudumisha ushirikiano na taasisi nyengine za kikanda na kimataifa katika maeneo muhimu katika kufikia malengo ya Kituo;
(h) kutoa miongozo ya ada kwa wasuluhishi na wapatanishi
(i) kupanga utoaji wa msaada kwa watu pale itakapohitajika;
(j) muda hadi muda kutunga Kanuni za Usuluhishi na Upatanishi chini ya Sheria hii na kupendekeza mabadiliko katika Kanuni;
(k) kufanya tafiti, kutoa elimu kwa umma na kutoa machapisho juu ya aina zote za njia mbadala za utatuzi wa migogoro;
(l) kuweka ofisi za Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro katika ngazi za Mikoa kama ambavyo Bodi itaona inafaa; n.k.

Tume ya Kutekebisha Sheria inapendekeza, Sheria itakayotungwa iweke kifungu chenye kukipa uwezo Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar kufungua vituo visaidizi ambavyo vitafanya kazi za kutatua migogoro katika mikoa

mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kuwepo kwa vituo hivyo kutasaidia kuondoa usumbufu kwa wananchi katika maeneo hayo ya mikoa, kuokoa muda na gharama.

**5.1.1.3 Kuanzishwa kwa Mfuko wa Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro**

Inapendekezwa kuwa Sheria itakayotungwa izingatie uanzishwaji wa Mfuko wa Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro. Lengo kuu la Mfuko huo ni kuwezesha shughuli mbali mbali za Ofisi kama vile kununua vitendea kazi, kutoa mafunzo endelevu kwa watatuzi wa migogoro, kufanya tafiti mbali mbali na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na njia mbadala za utatuzi wa migogoro, kuwezesha mazingira rafiki na salama kwa utendaji wa kazi za Ofisi n.k. Pia inapendekezwa kuwa Sheria iainishe vyanzo mbali mbali vya fedha ambazo zitaingia katika Mfuko huo. Miongoni mwa vyanzo vya Mfuko huo, inapendekezwa vijumuishe:

a) kiasi chochote cha fedha kama kitakavyokadiriwa na Baraza la Wawakilishi;
b) malipo yatokanayo na ada na tozo nyengine zinazolipwa chini ya Sheria hii;
c) fedha na mali nyengine zinazokusanywa na Ofisi kutoka vyanzo vyengine kwa njia ya michango na ruzuku; na
d) chanzo chengine chochote cha fedha.

**5.1.1.4 Watatuzi wa migogoro kutokuingiliwa utendaji wao na maamuzi wanayoyatoa**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro itambue uhuru wa watatuzi wa migogoro katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuweka kifungu maalumu ambacho kitamzuia mtu yeyote kuingilia utendaji wa mujukumu ya mtatuzi wa migogoro hadi kufikia kutoa

maamuzi, isipokuwa mahkama pale inapoona inafaa kufanya hivyo. Kuwepo kwa kifungu hicho katika Sheria kitawezesha kuimarika kwa maadili katika kazi, kufanya kazi kwa umakini na kujiamini, na kuwepo kwa usimamizi bora wa haki kwa wahusika wa mgogoro.

**5.1.1.5 Watatuzi wa migogoro kupewa uwezo wa kuitisha kielelezo au waraka wowote unaohusina na mgogoro**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa miongoni mwa mambo ya msingi ambayo Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar inapaswa kuzingatia ni pamoja na kuweka kifungu maalum katika Sheria hiyo kitakachowapa uwezo watatuzi wa migogoro, kuitisha waraka au kielelezo chochote ambacho wanaona kinafaa na kusaidia katika mchakato mzima wa utatuzi wa migogoro ambayo inaletwa mbele yao. Kuwepo kwa kifungu ambacho kitatoa uwezo huo kwa watatuzi wa migogoro katika Sheria hiyo na kutawafunga wahusika wa mgogoro wanaokataa kuwasilisha vielelezo au nyaraka wakati wa utatuzi wa migogoro hiyo.

**5.1.1.6 Kuweka wajibu kwa wahusika wa mgogoro katika kufuata miongozo ya utatuzi wa migogoro**

Inapendekezwa kuwa Sheria itakayotungwa izingatie kuweka wajibu kwa wahusika wa mgogoro ikiwa ni pamoja na kufuata amri na miongozo ya uendeshaji mzima wa shauri husika. Aidha, inapendekezwa kuwa pande zinzohusika katika mgogoro zitakiwe kuchukua jitihada za kuwajibika katika kutii miongozo mbali mbali ya kiutaratibu, kiushahidi na mambo mengine bila ya kuchelewa. Pamoja na hayo,

pande zinazohusika zitakiwe kutocheleweshа, kusababisha kuchelelewesha au kuzuia tuzo kutolewa.

**5.1.1.7 Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro kutokuingilia mifumo ya kimahkama**

Tume inapendekeza kuwa Sheria itakayotungwa isiweke masharti ambayo yatakuwa na mfanano ulio sawa na masharti ya utatuzi wa kesi katika mahkama. Utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala hufuata misingi na taratibu maalum ambazo huwa ni tofauti na zile taratibu zinazotumika mahakamani. Hivyo, Sheria iweke masharti bora ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro ambayo msingi wake unatokana na makubaliano ya wahusika wa mgogoro.

**5.1.1.8 Kuweka kifungu maalum katika Sheria kitakachowashurutisha wananchi kutatua mizozo yao kwa kuanzia na njia mbadala za utatuzi wa migogoro**

Tume inapendekeza Sheria itakayotungwa kuweka kifungu maalum ambacho kitawataka wananchi kutatua mizozo yao kwa njia mbadala za utatuzi wa migogoro kabla ya kupeleka madai yao mahakamani. Kutumia njia hizi mbadala za utatuzi wa migogoro kunaweza kupelekea wahusika wanaozozana, kufikia suluhisho la pamoja, hali ya kuwa kila mmoja ameridhika na kuafikiana na maamuzi. Vile vile, kuwepo kwa utaratibu huu kutasaidia kupunguza msongamano wa kesi katika mahakama za Zanzibar na hivyo, kutapelekea usimamizi bora wa haki ambazo zitapatikana ndani ya wakati.

#### 5.1.1.9 Upatanishi (Mediation) kutokutawaliwa na utaratibu ulio rasmi (too formal)

Tume pia inapendekeza kuwa Sheria itakayotungwa isiweke vifungu ambavyo vitafanya utatuzi wa migogoro kwa njia ya Upatanishi kuwa na mfumo ulio rasmi. Msingi wa aina hii ya utatuzi wa migogoro ni kusimamia kwa kuwapatanisha wahusika na kuwaongoza kufikia hali ya kupatikana kwa maamuzi ambayo yanatokana na makubaliano yao wenyewe. Hivyo, masharti ya Sheria itakayotungwa kuhusiana na Upatanishi, yasionekane kuwa katika mfumo rasmi na kuwabana wahusika.

#### 5.1.1.10 Sheria itakayotungwa kutambua ushahidi wa kielektroniki

Tume inapendekeza kuwa Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar itambue uchukuaji ushahidi kwa njia za kisasa za kielektroniki. Kutokana na mabadiliko na ukuaji wa kasi wa sayansi na teknolojia, ni muhimu kwa watatuzi wa migogoro kuekewa mifumo ya kisheria iliyokuwa imara na salama ya kuchukuwa ushahidi kwa njia za kielektroniki ili kuendana na kasi ya mabadiliko hayo. Utaratibu huu utarahisisha usikilizaji wa migogoro hata pale wahusika au mashahidi wao watakapokuwa nje ya Zanzibar au katika mazingira ambayo kutakuwa na makatazo ya watu kukutana kama ilivyokuwa wakati wa janga la Uviko 19.

#### 5.1.1.11 Sheria iweke utaratibu au muongozo maalum wa kufuatwa katika kutatua migogoro.

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa Sheria itakayotungwa iweke utaratibu maalum na wa pamoja ambao kila chombo chenye mamlaka kisheria kutatua migogoro, kitalazimika kufuata utaratibu huo. Utaratibu huo utakaowekwa,

ubainishe muda wa kusikiliza mgogoro hadi kumalizika kwake na kutoa maamuzi, kwa mfano utatuzi wa mgogoro katika upatanishi usizidi miezi sita badala ya muda uliozoeleka wa siku thelathini ambao unaonekana ni mdogo katika upatanishi, mawakili kuendelea kuruhusiwa kuingia katika upatanishi (mediation), kufungua shauri nje ya muda, na msuluhishi kupewa uwezo kisheria kumuita mtu yeyote ambae ataona anafaa na kusaidia katika kutatua mgogoro.

**5.1.1.12 Sheria ibainishe utaratibu wa kuwasilisha Ombi na kuanza kwa Usuluhishi wa ndani na wa kimataifa**

Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza, Sheria itakayotungwa ibainishe utaratibu wa kuwasilisha Ombi la Usuluhishi kwa kueleza kuwa Ombi hilo liwasilishwe kwenye Kituo cha Usuluhishi Zanzibar na kupelekwa kwa mlalamikiwa. Sheria ieleze Ombi la Usuluhishi lijumuishe:

i. madai kwamba mgogoro huo upelekwe kwenye Usuluhishi chini ya Sheria hii.
ii. majina, anuani, simu, baruapepe na namna nyengine ya mawasiliano ya wahusika wa mgogoro na ya mwakilishi wa mlalamikaji;
iii. nakla ya makubaliano ya Usuluhishi, na kifungu cha Sheria ambacho watakichagua ikiwa kitahitajika kutumika;
iv. maelezo mafupi na hali ya mgogoro, ikijumuisha viashiria vya uwepo wa mali na haki;
v. maelezo ya fidia inayoombwa na kiwango kinachodaiwa kwa kadri itakavyowezekana;
vi. mapendekezo yoyote yanayohitajika, na uchunguzi wowote ambao mlalamikaji anaona ni muhimu;

**5.1.1.13 Kurekebishwa kwa Sheria ya Mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza, Sheria ya Mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994 kufanyiwa marekebisho kwa kuondosha taratibu za uendeshaji wa mashauri kwa misingi ya Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8. Kwa mujibu wa kifungu cha 15 ya Sheria ya Mahkama ya Ardhi (Marekebisho) ya 2008, utaratibu wa uendeshaji wa mashauri mbali mbali unaotumiwa hivi sasa katika Mahkama ya Ardhi hufuata misingi iliyomo kwenye Sheria ya Mwenendo wa Madai, badala ya kutumia utaratibu wa kusuluhisha migogoro ya ardhi kwa njia za usuluhishi, upatanishi, mazungumzo na maridhiano. Kwa msingi huo, ipo haja ya kurekebishwa tena Sheria ya Mahkama ya Ardhi ili iendane na madhumuni hasa ya kuanzishwa kwa Mahkama hiyo.

**5.1.1.14 Sheria itambue suala la uwakilishaji wa wahusika wa mgogoro**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza, Sheria itakayotungwa iweke vifungu maaalum vitakavyoeleza suala zima la kuwawakilisha wahusika wa mgogoro katika upatanishi (mediation) na usuluhishi (arbitration) wa ndani na wa kimataifa. Sheria iwape fursa wahusika wa mgogoro kuchagua muwakilishi chini ya Sheria hii bila ya kujali utaifa au sifa zao za kitaaluma. Sheria ieleze wazi kuwa majina, anuani, simu, baruapepe na taarifa nyengine za mawasiliano za wawakilishaji ziwasilishwe katika Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro na upande mwengine wa mgogoro. Aidha, Sheria hii ieleze, kila muhusika wa mgogoro ahakikishe kuwa muwakilishi wake ana muda wa kutosha ambao utawezesha upatanishi au usuluhishi kumalizika kwa haraka.

**5.1.1.15 Kuwakilishwa kwa muhusika katika Usuluhishi endapo atafariki, kufilisika au kumalizika kwake (winding up)**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa, Sheria itakayotungwa itambue umuhimu wa kuendelea na taratibu na hatua za Usuluhishi hata katika mazingira ambayo muhusika wa mgogoro amefariki, amefilisika au kumalizika kwake (winding up). Katika kuendelea na mchakato wa Usuluhishi, Sheria hii iweke kifungu ambacho kitatoa mamlaka kwa wawakilishi wa wahusika hao kuendelea na taratibu zote hatua kwa hatua mpaka kumalizika kwa Usuluhishi na kutolewa tunzo.

**5.1.1.16 Watatuzi wa Migogoro kuzingatia maadili**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza, Sheria itakayotungwa iweke vifungu maaalum vitakavyoeleza suala zima la kuzingatiwa maadili kwa watatuzi wa migogoro kwani ni suala muhimu katika utatuzi wa migogoro. Aidha Sheria ielezee mambo ambayo yakitokezea mtatuzi wa migogoro anaweza kuondolewa katika orodha ya wasuluhishi wanaotambuliwa na Kituo pamoja na kuchukuliwa hatua ikiwemo hatua za kinidhamu au kufutiwa leseni ya kutekeleza masuala ya utatuzi wa migogoro.

**5.1.1.17 Msuluhishi kupewa uwezo wa kutoa uamuzi wa mpito**

Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza, Sheria itakayotungwa iweke kifungu maalum ambacho kitampa uwezo msuluhishi wa mgogoro kutoa uamuzi wa mpito endapo ataombwa na mmoja ya wahusika wa mogogoro huo. Sheria ibainishe wazi kuwa uamuzi huo wa mpito ni sharti utolewe kabla ya kumaliza kusikiliza mgogoro

husika na pia uwe ni wenye kulinda kitu kinachobishaniwa ikiwa kusubiri maamuzi ya mwisho kunaweza kuathiri kitu hicho au upande mmoja wa mgogoro husika.

**5.1.1.18 Sheria iainishe makosa na adhabu**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza, Sheria itakayotungwa iweke vifungu maaalum vitakavyoeleza makosa na adhabu. Vifungu hivyo vya adhabu vielezee juu ya mambo ambayo msuluhishi akiyatenda itakuwa amefanya makosa na ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria. Mfano wa vitendo hivyo ni pamoja na kushindwa kusimamia maslahi ya mteja au kumtelekeza, kwenda kinyume na matakwa ya mteja, kudharau kumuwakilisha ipasavyo, kufanya vitendo vya rushwa na kufanya matendo mengine yaliyo kinyume na utaratibu wa kisheria.

Aidha adhabu zinazopendekezwa zijumuishe kusimamishwa kwa leseni ya kufanya usuluhishi kwa muda au kufutiwa kabisa.

**5.1.1.19 Kituo kiweke viwango vya tozo na ada za utatuzi wa migogoro**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza, Sheria itakayotungwa iweke vifungu maaalum vitakavyoeleza utaratibu wa uwekaji wa viwango vya tozo na ada kila baada ya muda itakayolipwa kwa ajili ya utatuzi wa migogoro. Suala hili litasaidia kuepusha tatizo la watatuzi wa migogoro kujipangia viwango vikubwa vya ada wanavyotaka na kupelekea wananchi kushindwa kumudu gharama hizo na kufanya wananchi kukimbia njia mbadala za utatuzi wa migogoro.

**5.1.2 Mapendekezo yasiyo ya Kisheria/kiutendaji**

#### 5.1.2.1 Kutungwa kwa sera maalum itakayojulikana kama Sera ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar

Muda umefika sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia vyombo vyake husika kutunga sera maalum inayohusiana na masuala ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbalada nchini Zanzibar. Sera hiyo itakayotungwa itoe mwelekeo kwa vyombo husika kuweka taratibu za kisheria na kutoa suluhisho kwa mizozo inayoibuka katika nyanja mbali mbali za Kibiashara, Kazi, Uchumi, ikiwemo uchumi wa Buluu na Uwekezaji kwa ujumla. Aidha Sera hiyo izingatie taratibu mbali mbali za kiutendaji, kuweka miongozo na kutoa mwelekeo juu ya namna bora za kutatua migogoro katika ngazi za kitaifa na kimataifa.

Uwepo wa Sera hiyo ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar, utatoa mwelekeo wa namna bora ya utungwaji wa Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar, kwani sheria husika hufuata mwelekeo wa sera ambayo hutoa taaswira nzima ya taifa linapoelekea.

#### 5.1.2.2 Suala la Utungaji wa Kanuni

Katika kuhakikisha masuala ya utatuzi wa migogoro kwa kutumia njia mbadala linatekelezwa ipasavyo, Tume inapendekeza kutungwa kwa kanuni ambazo zitaelezea kwa undani taratibu za utatuzi wa migogoro kwa kutumia njia mbadala. Kanuni hizo zinatarajiwa kuweka maelezo ya kina ambayo yamewekewa misingi katika Sheria ili Sheria hiyo iweze kutekelezeka. Kanuni pamoja na mambo mengine itafafanua kuhusiana na utaratibu wa kusikiliza migogoro, viwango vya ada

itakayotozwa na Kituo, utaratibu na vigezo vya upatikanaji leseni, kufutwa na kusimamishwa kwa leseni, na mambo mengine ambayo Sheria imeeleza.

**5.1.2.3 Wajibu wa kutoa elimu juu ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro kwa wananchi.**

Wananchi wengi wanaonekana kukosa uelewa wa kutosha kuhusiana na njia mbadala za utatuzi wa migogoro pamoja na taratibu zake. Kawaida wananchi hao hufahamu taratibu za kufungua mashauri ya madai yao mahkamani pale wanapokuwa na migogoro kutokana na kutofahamu fursa za kisheria za kutatua mizozo yao kwa njia za mazungumzo, upatanishi au usuluhishi ambazo zinaweza kusimamiwa na vyombo vyengine visivyokuwa mahkama. Hivyo, inapendekezwa kuwa taasisi itakayopewa jukumu la kusimamia Sheria hii, ichukue jukumu la kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro. Kwa msingi huo, Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar kiwe na wajibu wa kusimamia taratibu zote za kutoa elimu kwa wananchi.

**5.1.2.4 Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Zanzibar kiwe ni jengo lenye hadhi**

Kutokana na shughuli za Kituo cha Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro kutatua migogoro ya watu mbali mbali wakiwemo wafanya biashara, wafanya kazi na wawekezaji, ni muhimu jengo la Kituo hicho kuwa katika hali bora, na yenye hadhi. Kituo kiwe na kumbi za kutosha za kusikiliza madai ya wahusika wa migogoro, huduma za kimaktaba, kumbi za mikutano na hata maeneo ya kufanyia mafunzo. Hali hiyo haitaleta hamasa kubwa na imani kwa watu hao juu ya Kituo hicho tu, bali

hata kuleta ufanisi mzuri wa kazi kwa watendaji kufanya kazi katika mazingira mazuri yanayolingana na kazi wanazozifanya.

**5.2 Hitimisho**

Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro zinawezesha utatuzi wa mapema wa migogoro ambayo huibuka katika jamii, ambayo inatokana na  nyanja mbali mbali za kiuchumi, biashara, ajira n.k. Utatuzi wa mapema wa migogoro hiyo unaweza kuwa na manufaa na maslahi kifedha na kiuchumi kwa wahusika wa mgogoro huo. Aidha, kutumia njia hizi za utatuzi wa migogoro kunaweza kupelekea kurekebishwa na kudumishwa kwa uhusiano baina ya wahusika wa mgogoro.

Mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa kutumia njia mbadala ni vyema kuonekana kama ni sehemu muhimu ya mfumo wowote wa kisasa wa haki ya raia. Jambo la kuzingatia ni kwamba wananchi wanapaswa kupewa fursa za kuchagua katika kutatua migogoro yao kwa njia ambayo inahitaji zaidi maslahi na malengo yao. Jamii inapaswa kuwa na mfumo jumuishi wa haki za kiraia ambapo Mahakama huwa ni jukwaa la uamuzi wa mwisho likisaidiwa na mbinu nyingine zinazohusiana kwa karibu ili kuhakikisha kuwa sheria iko wazi kwa wote.

Kutokana na mabadiliko ya maendeleo ya kiuchumi na kibiashara ulimwenguni sambamba mwelekeo wa Zanzibar katika kuimarisha sekta za viwanda, ajira, biashara, uwekezaji na uchumi, wakati umefika sasa Zanzibar kutunga sheria itakayojikita katika kutatua migogoro mbali mbali inayoibuka katika sekta hizo kwa njia mbadala, kabla ya migogoro hiyo kupelekwa mbele ya Mahkama. Kufanya hivyo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini

kwa wawekezaji kujenga imani na mfumo wa utatuzi wa migogoro pale inapojitokeza. Aidha mfumo huo wa utatuzi wa migogoro utaokoa muda na fedha, na pia kuisaidia Mahkama kwa kuiondoshea mzigo wa kusikiliza mashauri mengi ambayo yangeweza kutatuliwa kwa njia nyengine za utatuzi wa migogoro kama vile upatanishi, usuluhishi n.k.

**SERA NA MIPANGO**

Sera ya Uwekezaji Zanzibar ya 2005

Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020

**SHERIA ZA ZANZIBAR**

- Sheria ya Usuluhishi Sura ya 25
- Sheria ya Usuluhishi (Tuzo za Kigeni) Sura ya 27
- Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8
- Sheria ya Mahkama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994
- Sheria ya Mahusiano Kazini Nam. 1 ya 2005
- Sheria ya Mahkama ya Biashara Zanzibar (Divisheni ya Mahkama Kuu) Nam. 9 ya 2013
- Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017
- Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar Nam. 4 ya 2021

**MIKATABA YA KIMATAIFA**

- Sheria ya Masharti ya Usuluhishi (Itifaki) Sura ya 26
- Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter) wa 1945
- Mwongozo wa Kisheria wa Tume ya Kimataifa ya Biashara ni ya Umoja wa Mataifa (UNCITRAL) 1985
- Mkataba uliorekebishwa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) wa 1993

- Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wa 1999
- Sera ya Uwekezaji ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi ya 2018
- Chama cha Usuluhishi cha Afrika

**SHERIA NA UZOEFU WA NCHI MBALI MBALI**

- Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro Nam. 30 ya 2007 ya Samoa
- Sheria ya Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 37 ya 2008 ya Mauritius
- Sheria ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro ya 2010 ya Ghana
- Sheria ya Kituo cha Nairobi cha Usuluhishi wa Kimataifa Nam. 26 ya 2013 ya Kenya
- Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania Bara Nam. 2 ya 2020
- Mahkama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya Ufaransa
- Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro cha London

**TOVUTI**

- https://www.lawreform.ie/_fileupload/consultation%20papers/cpadr.pdf
- https://www.arbitrage.org/caip/?lang=en
- https://www.idrc.co.uk/
- https://www.idrc.co.uk/virtual-hybrid-hearings/
- https://www.legalserviceindia.com/legal/article-2308-introduction-to-the-concept-of-alternative-dispute-resolution.html
- https://www.un.org/en/about-us/un-charter
- https://www.wipo.int/amc/en/arbitration/what-is-arb.html
- https://ecowas.int/ecowas-law/treaties/

- https://www.eac.int/overview-of-eac#:~:text=The%20East%20African%20Community%20(EAC,its%20headquarters%20in%20Arusha%2C%20Tanzania.
- https://www.mea.gov.in/Portal/ForeignRelation/east-african-community-april-2011.pdf
- https://en.wikipedia.org/wiki/World_Intellectual_Property_Organization
- African Arbitration Association (AfAA) and International Arbitration in Africa – The Arbitrator
-